

MSIOGOPE

 Endeleeeni kusimama kwa dakika moja tunapoinamisha vichwa vyetu mbele za Bwana na kuomba. Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, sijui ni wangapi hapa ndani wangetaka kukumbukwa katika maombi mbele za Mungu, inua tu mkono wako, na haja yako moyoni mwako. Na tuombe.

² Baba mwenye rehema na Mtakatifu, Mungu, tunakuja kwa unyenyekevu Uweponi Mwako tukiwa na shukrani mioyoni mwetu, kwa sababu kwamba Wewe ulitupenda sana, hata ukamtoa Mwanao wa pekee, ili kila aaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele.

³ Ee Mungu, kuna wale ambao wamepokea baraka hii kuu ya ahadi, jinsi tulivyo na shukrani, Bwana, na mioyo yetu inawaka kwa ajili ya wengine kupokea furaha hii isiyoneneka na iliyojaa utukufu ambayo imetolewa kwa jamii ya binadamu.

⁴ Kuna wale walio wagonjwa na wahitaji usiku wa leo, Baba, wamelala hapa wanateseka, na wamepigwa, na wameshambuliwa, na, Mungu, ni ulimwengu mgonjwa, bali Wewe ulitufanyia maandalizi, Bwana, kwa maana imeandikwa, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.”

⁵ Sasa, Baba, sisi ni watumishi Wake tu hapa, tukijaribu kuwapa watu Neno Lako, na ili waweze kuona, na kufahamu, nasi tunajua ya kwamba mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio. Na ulifanye halisi sana kwa kusanyiko, usiku wa leo, hata hakutakuwako na mtu mnyonge miongoni mwetu ibada itakapokwisha, kusiwe na mwenye dhambi mmoja, wote waokoke, ndani na nje, vitanda vya wagonjwa na viwe vitupu, viti vya magurudumu viwe tupu, kila mtu aliye na ugonjwa wa moyo, kansa, anayekufa.

⁶ Jalia kuwe na wakati wa yubile kote mjini na kote kote bondeni, kuibuke uamsho wa mtindo wa kale ambao utaenea huku na huku pwani hii, Bwana, kwa sababu ya Uwepo Wako, usiku wa leo. Iimarisha mioyo yetu na imani yetu Kwako, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

⁷ Mnaweza kuketi. Ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makubwa ya kuwa hapa katika ukumbi huu kwenye uwanja wa maonyesho, usiku wa leo, nami nilisikitika kwamba jana usiku jinsi ilivyotubidi kukurupuka na kuharakisha moja kwa moja kwa sababu ya tahadhari kwenye lile ghala la silaha, wala hata hatukuweza kupata msingi.

⁸ Mnamjua adui yetu mkuu, ibilisi, na kama hawezi kutushika kwa njia moja, atajaribu nyingine. Kama sote tunaweza

kuwaleta watu katika nia moja, basi ameninii, hawezi kusumbua hilo, kwa hiyo basi atafanya jambo lingine kuuvuruga mkutano kwa njia nyingine, kusudi tusiweze kabisa kutulia, na kusikiliza, na kuangalia, na kuamini, kisha tuone matendo ya Bwana.

⁹ Ninashukuru sana kwa ajili ya ukumbi huu, usiku wa leo. Samahani kuona mamia ya watu wamesimama, lakini sisi tu, ni, nina hakika shirika hili linafanya yote wajuayo jinsi ya kufanya ili kutoa nafasi kwa watu ku—kuketi.

¹⁰ Na sasa, ninaamini kama huu ukiendelea hivi, inastahili kujaribu tena. Hivi hamwoni hivyo, jamani, kujaribu tena? Mbona, labda tunaweza, tunaweza kupata hema na kuliweka hapa nje, mahali fulani, ambalo litaketi watu ishirini, thelathini elfu, na kuliacha tu likae kwa majuma matatu au manne, nasi kweli tupate kufahamiana na kujuana, ili kwamba... Na kama Bwana akipenda, hilo ndilo tunalohitaji, tutakaloninii, kunikaribisha, nami ninathamini hilo, na kama hayo ni mapenzi ya Bwana.

¹¹ Daima ni—ninataka kufuata mwongozo Wake, mahali tu anapoenda, anapoongoza, na ndipo tunajua tuko sahihi. Hebu niwaambie ni kwa nini: Kama ukiingia katika matatizo mahali fulani, na halafu kama huna hakika ya mwongozo wako, basi Shetani anaweza kusema, “Vema, unaona, hili *hapa*.”

¹² Lakini kama unajua unaongozwa, unaweza kukutana naye moja kwa moja tena, na kusema, “Nimekuja katika Jina la Bwana,” unaona, “kwa hiyo rudini tu nyuma! Hivyo tu.” Mnaona? Naye itambidi kufanya hivyo kama—kama Bwana alikutuma. Huko nje katika nchi za kigeni, ninapoenda huko ambako tuna wachawi wengi sana na kadhalika wa kushindana nao, ambapo wakati wowote unajua ya kwamba unaongozwa kufanya jambo hilo, Roho Mtakatifu alikuchagua kulifanya, vema, upinzani si kitu basi, unakaa moja kwa moja uwanjani, unakaa papo hapo na kusonga mbele mpaka ushindi utakapokuja.

¹³ Na kwa hiyo, usiku wa leo, ninatumaini ya kwamba sitawaweka kwa muda mrefu sana, mimi. . . kwenye somo dogo la Maandiko, na ndipo mimi. . . Tutakuwa na wakati mgumu sana kufanya mstari wa maombi, naona, huku milango yote miwili imeegemezwa kuwaleta hao. Wote walio na kadi hizi za maombi, zishikilieni. Nawaambia katika hali hizi, wakati mwingine. . .

¹⁴ Nilitoka nje ndipo kijana mmoja akaniambia, akasema, “Ndugu Branham, wamejaa sana humu ndani kadiri tu walivyokuwa mahali pale pengine.” Kasema, “Hatuna nafasi.”

¹⁵ Nikasema, “Vema, jinsi tu ninavyoweza. . .” Kwa kweli, nipo hapa kwa kusudi moja, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, hilo ndilo la kwanza; na kwa ajili ya wokovu wa nafsi, la pili; na kujaribu kuona wagonjwa wakiponywa, la tatu. Kwa

hivyo hiyo ni . . . Nami sikuja kuwachukua wagonjwa wa daktari, la, nimekuja kuwaombea wagonjwa wa daktari, washiriki wa mchungaji, marafiki zangu, mnaona, na kuwaombea tu.

¹⁶ Na sasa, nilifikiri labda tungekuwa hapa, Jumapili, ni ibada ya alasiri, kwa hiyo kutakuwa na joto wala watu hawatajali, labda, wakisimama nyuma huko nje. Lakini kama usiku wa leo na kesho usiku kama tunaweza kuleta ninii, kwa neema ya Mungu kupitia Neno la Mungu, utambuzi wa Uwepo wa Mungu, mnaona, ndipo tunapoanza mstari halisi wa maombi, wawekeni mstarini waliojeruhiwa, *wowote wale*, wa kuombewa, ninaamini basi tutapata matokeo. Mnaona?

¹⁷ Kwa maneno mengine, ni kujenga, kama vile mhudumu alivyotoa somo lake kwenye somo fulani, kisha kuelezea, somo lake, akilishindilia; seremala akiweka ubao wake, kisha akaupigilia misumari. Na hilo ndilo tunalotaka kujaribu kufanya, kwa sababu hatuna sababu ya kuwa hapa kama haikuwa ni kujaribu kufanya jambo fulani kuwasaidia watu, hiyo ndiyo sababu tuko hapa.

¹⁸ Mimi . . . Kama—kama uponyaji . . . Kama, kijana huyu aliyelala hapa kwenye machela hii, maskini kipenzi huyo wa thamani, aliyeketi hapo kwenye kiti cha magurudumu, kitoto kidogo, maskini mama huyu aliyelala hapa kwenye machela, yule mama aliyeketi pale kitini, kitu fulani, mtu fulani huko nje anayekufa kwa ugonjwa wa moyo, mama fulani aliyeliwa na kansa, mbona, kama ningeweza kufanya lolote kuwasaidia, mimi, si ningekuwa mhudumu duni kama ningeweza kufanya jambo fulani wala—wala silifanyi? Sina mahali huku nyuma, enyi marafiki, kama ningekuwa hivyo. Kama ningeweza . . . Ninasema jambo hili, linasikika kuwa halina maana, lakini kama ningeweza kuchukua ro—robo na kuisukuma kwa pua yangu kupitia kwenye mji huu nipate kumponya mtu fulani, ningelifanya, mnaona, ningelifanya. Ninajua maana ya kuwa mgonjwa, mimi mwenyewe nimekuwa mgonjwa.

¹⁹ Halafu basi nimeona ambapo daktari alisema ya kwamba kamwe nisingeweza kuwa mzima wala kamwe sitaishi, kisha nikapata *kitu* hata ninaishi, na—nataka kumwambia kila mtu kukihusu, mnaona. Na sasa, ndipo naja kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu jinsi Yeye angefanya, alivyosema, ambapo tungeweza tu kupata matokeo bora sana katika maskini muda huu mfupi tulio nao.

²⁰ Sasa, kweli inachukua muda mrefu zaidi kukaa mkutanoni kuliko vile tunavyofanya hapa, kwa sababu mara nyingi watu huingia haraka, nao hawaelewi, kisha wanatoka nje ndipo—ndipo hisia ndogo ya kwanza ya kigeni waliyo nayo, haidhuru unajaribu kuwaambia watu jinsi gani, wa—wangali watategemea hisia zao, wao ni, ni moja tu ya hisia zao wanazotumia, “Nikijisikia vizuri zaidi, nitaliamini.” Mnaona?

Lakini hiyo haina uhusiano wowote nalo. Basi kama tunaweza kuwa hapo muda mrefu vya kutosha tukikutana na watu kuwafanya waone ukweli wake ni nini, na jinsi ya kudumu pamoja na Mungu, basi mtapata matokeo mazuri, ni wakati unapofanya hivyo.

²¹ Kwa hiyo sasa, ninatumaini ya kwamba mtadumu pamoja nami, na kujua ya kwamba niko chumbani mwangu nikiomba na kumtafuta Mungu kila saa niwezayo, kujaribu kufanya niwezalo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu na kwa ajili yenu, wakati nikiwa hapa pamoja nanyi.

²² Na sasa, sasa, kesho usiku, kumbukeni na halafu, sasa, kama—kama kadi zenu za maombi hazijaitwa, zishikilieni, tunawajibika kuwaombea wagonjwa tunaowapa kadi za maombi, kwa hiyo tu—tunawajibika kimaadili kufanya hivyo, nasi tutafanya hivyo kwa neema ya Mungu, na kila mtu kama kweli tukiweza, mnaona, hiyo ndiyo—ndiyo nia.

²³ Sasa, kama tungekuwa hapa ninii kadha, labda majuma mawili au matatu, vema, tungeanza tu kupata *kadha* wa *kadha*, hatimaye tungeweza kuyachimbua moja kwa moja, lakini kama—kama. . . Tutajaribu tusigawe kadi nyingi sana za maombi, bali kadiri tu tuwezavyo, tunaofikiri tuna wakati wa kutosha kuwachukua, kuwachukua wengi tuwezao usiku kucha.

²⁴ Sasa, nilitaka kusema jambo fulani jana usiku, hili linasikika la kigeni katika mji mwingine, mimi huweka suti zangu kwa dobi zikapigwe pasi, nami nimeishi nikisafiri mahali mahali kwa karibu miaka kumi na mitano sasa, suti zinakunjamana, ndipo ikanibidi kupeleka suti zangu mbili huko chini zikapigwe pasi. Na—na kama maskini wasichana hao waliolipia kazi hiyo ya kupiga pasi wapo hapa, nawashukuru, enyi dada.

²⁵ Nilingia, hawangeniruhusu niilipie, kasema dada wawili waliokuwa pale walikuwa wameilipia; naye huyo mama akasema walikuja wakiisugua suti yangu. Sasa, hilo ni zuri sana, na—nathamini hilo, hilo lapendeza kweli. Lakini bila shaka, ninii ya—yao. . . hiyo ilikuwa ni suti tu, lakini ninatumaini ya kwamba kama mlitaka kitu fulani, Mungu ataiheshimu imani yenu, mnaona, kwa—kwa kufanya hivyo, mnaona, bali ilikuwa ni suti tu. Kwa hiyo, ninathamini imani ye—yenu na kuamini ya kwamba angalau ningewaambia, kuwaambia ukweli nipate kuwa mwaminifu kwenu, basi asanteni sana.

Nikamwambia huyo mama, “Acha niwape hiyo pesa.”

Kasema, “La,” kasema, “la,” kasema, “wa—wasingevumilia hilo.”

Kwa hiyo kama uko hapa, “Asante.” Ilikuwa ni Star Cleaner huko chini kwenye u—u—ule mji tulimotoka.

²⁶ Sasa, ni—niliwazia, usiku wa leo, somo la mkutano wa ushuhuda kutoka katika Biblia, nami ninataka kusoma kwa ajili ya somo kutoka katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 14, kifungu cha 27.

Ndipo mara Yesu akasema nao, akawaambia, *Jipeni moyo; ni mimi; msioCOPE.*

²⁷ Sasa, ninataka kuchukua somo *Msiogope* kwa ajili ya mkutano huu wa ushuhuda.

²⁸ Kuna vitu viwili vinavyoitawala jamii yote ya mwanadamu ulimwenguni, kimoja ni hofu, kingine ni imani. Sasa, ama ni hofu au imani inayotawala kila taifa, kila dhehebu, na kila mtu binafsi, wewe, unatawaliwa ama na hofu au imani.

²⁹ Sasa, hapana shaka ilikuwa yapata kutua kwa jua, jua lilikuwa likitua, na maskini ule mtumbwi ulikuwa umezama kwenye fuo kwa sababu wanafunzi walikuwa wamepanda humo. Naye yule mtu mkubwa mwenye nguvu, ambaye tunaamini kuwa ni Simoni, yule mvuvi, akiwa na uzoefu mzuri wa mashua, na ziwa la kuvuka, kazi yake ilikuwa ni kuvua samaki, na sasa, alipoanza kuchukua mikono yake mikubwa, yenye misuli migumu, na huku nyuma akisukuma maskini huo mtumbwi kutoka ukingoni, akapanda, akaketi karibu na ndugu yake, Andrea, akachukua makasia yake.

³⁰ Katika siku hizo mashua zilikuwa zikiendeshwa ama kwa—kwa kupiga makasia, au kupuliziwa kwa matanga; nami ninaamini ya kwamba wakati mwingine walipiga makasia, endapo kulikuwa na upepo mkali, wangeweza pia kupandisha matanga.

³¹ Na ha—hapana shaka kulikuwako na karibu umati kama huu, na huko ukingoni wakipunga mikono, loo, ninamaanisha msongamano kama huu, lakini labda mara nyingi kuliko huu. Nafikiri kulikuwa na yapata elfu tano, nao walikuwa wamesimama ukingoni wakipunga mikono, walikuwa wakiwaaga watumishi hawa wa Kristo, kwaheri.

³² Sasa, ninaamini kama tukifanya hii mfano wa masimulizi, mpate kuona ya kwamba siyaondokei Maandiko. Maandiko ndiyo tunayoamini, na wakati Mungu ametoa ahadi, basi Mungu hana budi kudumu na ahadi Yake; hawezi kuiacha hiyo ahadi na abaki Mungu.

³³ Labda walipiga makasia umbali wa yadi mia chache, nao wangepiga kasia moja au mawili kwa makasia hayo ya mikono miwili. Na kama ilivyowabidi kufanya wakati huo, kwa namna fulani katika kazi ya pamoja, wakiivuta maskini hiyo meli kutoka kwenye...kusafiri, wakiendelea kuyapiga maji katika hiyo Bahari tulivu ya Galilaya, kwa kuwa utulivu ulikuwa juu ya hiyo bahari wakati wa machweo ya jua.

³⁴ Basi huko ufukoni watu walikuwa wakipunga mikono, wakiwaomba warudi tena, wawatembelee, ndipo ya mwisho ilipofifia, kwaheri ya mwisho, hapana shaka wanafunzi walipiga makasia kwa nguvu sana basi, wakijua walikuwa na mapambano kwelikweli kuvuka bahari hiyo usiku kucha, wapate kufika ng'ambo ya pili.

³⁵ Baada ya yapata, kwenye machweo ambapo wasingeweza kuwaona hao watu tena, hapana shaka kijana Yohana ndiye aliyeacha kupiga makasia, na, labda, kwa kuwa hakuwa na uzoevu wa makasia kama hao mabaharia wengine mabingwa walivyokuwa, akakoma, akarudisha nyuma nywele kutoka usoni mwake, na—na kuvuta pumzi kidogo, muda kidogo wa kupumua, kwa namna fulani wapate kuvuta pumzi kutokana na kupiga makasia kwa nguvu sana, wakijaribu kuvuka kadiri walivyoweza kabla giza halijaingia.

³⁶ Nami ninawazia walianzisha mkutano wa ushuhuda, na kijana Yohana hapana shaka alisema kitu kama hiki: “Ndugu zangu, baada ya leo, siamini kunaweza kuwa na yeyote wetu anayewazia ya kwamba tunamfuata mdanganyifu. Ninaamini, nionavyo mimi, Yeye alijithibitisha Mwenyewe, leo hii, kuwa kile hasa tulichomtarajia kuwa.

³⁷ “Aisee, hivi ninyi ndugu mlima, leo, wakati huo umati wa watu wenye njaa waliokuwa wamemzunguka kusikia Neno la Mungu...? Na kuona jinsi walivyosongamana, na kusukumana ili kukaribia, na baadhi yao hawakuwa wamekula siku nzima, nao hao mama jinsi walikwajuka pamoja na watoto wao wachanga, na kunyonya, na kadhalika, na wagonjwa wakisukumana pande zote!

³⁸ “Lakini wakati alipoomba hao samaki, ndipo nikamwona maskini mvulana huyo, naye akaleta maskini hizo biskuti tano ndogo, ama, vipande viwili vidogo vya samaki pale juu, naye akawaketisha wote chini hamsini-hamsini kwenye ubavu wa hicho kilima chenye nyasi, na mimi, mwenyewe, nikashangaa alilokuwa anaenda kufanya, huku akiwa tu na chakula kimoja kidogo cha mchana ambapo mvulana mdogo, labda, ametoroka shuleni, naye akausikia huo umati, ndipo akapanda mlimani kuona yaliyokuwa yakitukia, nao ulikuwa unavutia sana akasahau tu chakula chake cha mchana, alitaka kuona yale huyu Msemaji mkuu aliyokuwa akisema, aangalie yale aliyokuwa akifanya.

³⁹ “Basi nilipomwona akichukua mkate huo, hivyo vipande vidogo vya biskuti, akaviinua na kuvibariki, nilipomwona akiumeza mkate huo, na kuuweka mikononi mwetu sisi ndugu, na kunyosha mkono kuifikia biskuti iyo hiyo, na kuchukua kipande kingine cha biskuti, ndipo aliponyosha mkono tena, kulikuwa na kipande kingine cha biskuti tayari kimeota, na kuokwa, na kukolea, na tayari kwa kuliwa, mnajua nini, ndugu?”

Huenda alisema kitu kama hiki: “Tlinikumbusha juu ya hadithi za Biblia ambazo nilikuwa nikimsikia mama yangu akiniambia habari zake.

⁴⁰ “Nilipokuwa mvulana mdogo wa Kiyahudi, ninamkumbuka maskini mama yangu mrembo na jinsi alivyokuwa akiniambia, ‘Mpenzi, wakati watu wetu walipotoka Misri, tulikuwa watumwa wakati mmoja, na wakati tulipokuwa na nabii mkuu aliyeinuka miongoni mwetu, Musa, ambaye Mungu alimtuma kwetu apate kutuokoa na mateso yetu ya utumwa, naye Musa, bila shaka, asingeweza kuoka mikate, lakini tulipokuwa na watu milioni mbili na nusu huko nyikani, ambako hakukuwa na ngano, wala chochote, cha kutengenezea mikate, Yehova alimwaga mikate kutoka mbinguni kwa ajili yetu.’

⁴¹ “Nami nilikuwa nikishangaa, ningesema, ‘Mama, je, Yehova ana kundi kubwa la Malaika kule juu, na matanuri mengi sana ambayo Yeye huokea mikate Yake? Yeye alipata wapi mikate hii, Mama? Au hivi tungeweza kuangalia juu angani na kuona mioto kutoka kwenye tanuri Lake kila usiku walipokuwa wakiioa?’

⁴² “Mama labda angesema kitu kama hiki: ‘La, Mwanangu, wewe ni mdogo sana huwezi kuelewa, si lazima Yehova awe na matanuri, Yehova ni Muumba, Yeye huumba tu hiyo mikate, nayo inaanguka ardhini.’”

⁴³ Kijana Yohana, alipokuwa amesimama chomboni akiwashuhudia hao ndugu, akikiri imani yake kuu katika Yesu, alisema, “Hapana shaka alikuwa na uhusiano fulani na Yehova, kwa sababu Yeye aliumba mikate kama Yehova alivyoumba. Kwa hiyo kwangu mimi Yeye kweli ni Masihi, kwa sababu Yeye ni Mwana wa Mungu, Yeye—Yeye anaweza kuumba, na kuoka mikate, na—na kufanya tu kama Yehova alivyofanya. Kwa hiyo hilo lilitosha kwangu nilipomwona akiimega mikate hiyo na samaki hao, wala si samaki wabichi tu, bali ilikuwa ni samaki waliopikwa, tayari kwa kuliwa.”

⁴⁴ Ningetaka kuwauliza wasikilizaji wangu usiku wa leo: “Ni atomi ya namna gani aliyoifungulia basi, wakati alipokuwa na samaki waliopikwa na—na mikate iliyopikwa, na kuchukua biskuti tano na samaki wawili wadogo, na kuwalisha watu elfu tano, na kuokota vikapu vilivyojaa, masalio?” Yeye alifanya nini? Sayansi ingesema nini kuhusu hilo leo? Ni atomi ya namna gani, ama molekuli, ama chochote wanachotaka kuiita, inayoachiliwa basi?

⁴⁵ Lakini Yeye alifanya hivyo, naye maskini Yohana alishawishika kwamba hadithi za Biblia ambazo mama alimwambia kuhusu Yehova, Yehova yuyo huyo alidhihirishwa katika Mwanadamu, aitwaye Bwana Yesu Kristo, maana hakuna mtu mwingine angaliweza kufanya hivyo, Yeye alikuwa ni Muumba.

⁴⁶ Vema, Simoni, mnajua jinsi alivyo, daima yuko tayari kushuhudia. Na huyo ni kama Mkristo mwingine yeyote wa kawaida ambaye kweli anamjua Mungu, anamjua Bwana Yesu, yuko tayari kutoa ushuhuda wake, upesi sana. Na kama vile tulivyozungumza jambo fulani kumhusu jana usiku, huenda nikaurudia ushuhuda wake.

⁴⁷ Akasema, “Mbona, ndugu, nilipokuwa nikivua kwenye bahari hii hapa pamoja na baba yangu, miaka mingi iliyopita . . . Nami ninajua nyote mlimjua maskini baba yangu Mfarisayo, jinsi alivyokuwa mtu mashuhuri wa kanisa na alimwamini Mungu. Kila mara asubuhi kabla hatujaenda kuvua samaki, tulikutegemea tupate riziki, kwa hiyo angeniomba nipige magoti pamoja naye na kuombea hapa nje ufukoni kwa ajili ya samaki wetu wa siku hiyo, na Mungu kamwe hakutupungukia.

⁴⁸ “Ninakumbuka wakati nywele zake zilipoanza kuingia mvi, nami nikajua ya kwamba hivi karibuni itanibidi kuachana na baba yangu mzee, siku moja nakumbuka alinichukua, akaniketisha chini kwenye de—demani ya mtumbwi, kasema, ‘Simoni, mvulana wangu, ninataka ukumbuke hili: Israeli yote imekutarajia kuja kwa Masihi, na wakati unapokaribia, kila mtu daima amewazia angeishi kuona siku atakayokuja, nami niliwazia vivyo hivyo, lakini ninazeeka sasa, nami nadhani sitaweza kuiona. Lakini Simoni, kama mwaminio wa Biblia, kama mwaminio wa Yehova, ninataka kukupa funzo, mwanangu.’”

⁴⁹ Hilo ni jambo zuri la baba mkongwe kufanya, ama mama. Sijui kama, siku hizi, kama tunatumia wakati mwingi zaidi katika kuwafunza watoto wetu katika mambo ya Bwana, kuliko tunavyofanya kuhusu magari ya kasi na mambo mengine, tusingekuwa na uhalifu mwingi sana wa vijana, hiyo ni kweli.

⁵⁰ Susanna Wesley alikuwa mama wa watoto kumi na saba, hakuwa na mashine za kuosha vyombo za kubonyeza, na—na mifereji ya kufungulia apate kuchota maji, na hata hivyo pamoja na watoto hao wote angeweza kutumia saa mbili hadi tatu kwa siku katika maombi kuwazunguka hao watoto kumi na saba. Kutoka kwenye kiota hicho kidogo cha ndege wadogo kukatokea John na Charles, ambao waliuchochea ulimwengu. Tunahitaji akina mama zaidi kama hao, wenye wakati wa kuwafundisha watoto wao habari za Mungu.

⁵¹ Nilisimama karibu na kaburi lake si muda mrefu uliopita, huko London, nilipokuwa huko kumwombea mfalme, na nikisimama pale nimeweka mkono wangu juu ya kaburi lake, nikasema, “Mungu umpe raha mama huyo wa thamani, ninajua umempa.” Na hapo, aliyezikwa karibu naye, bila shaka, ni Bunyan, *Safari ya Msafiri*, na kadhalika, na William Cowper, halafu huko kwenye uwanja wa kanisa, amelazwa John, mabaki ya mwili wake mavumbini.

⁵² Ndipo Simoni akasema, “Baba alikuwa ameniambia mara nyingi, ‘Sasa, Simoni, mwanangu, kabla tu ya kuja kwa Masihi, kutakuwa na vurugu kubwa miongoni mwa watu, naye adui ataeneza ma—mambo mengi ya uongo, akiyaita Masihi. Nami nakutaka ukumbuke, Simoni, mvulana wangu, jinsi Masihi wa kweli atakavyokuwa, na jinsi atakavyoonekana, na jinsi atakavyokuwa. Masihi wa kweli atakuwa kulingana na Biblia, kulingana na yale manabii wetu wametwambia, Musa alisema, ‘Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii, kama nilivyo mimi.’”

⁵³ Naye hapana shaka alinyosha mkono akamgusa Andrea, akasema, “Andrea alienda kwanza kumsikia. Nisingeweza kuamini wakati yule, yale Yohana alikuwa kule chini akihubiri, akibashiri, kulikuwa na kuja kwa Masihi, kwangu mimi ilikuwa ni *uvumi* mwingine tu, lakini siku moja Andrea alikuja akaniambia ya kwamba ninapaswa kuja kumwona Mtu huyu, angalau nimsikilize mara moja, nami moyoni mwangu nilikuwa na yale baba aliyoniambia, halafu yale Maandiko yalikuwa yamesema ya kwamba Masihi huyu angekuwa Mungu-Nabii.

⁵⁴ “Ndipo nilipoingia kwenye kusanyiko pamoja na ndugu yangu, Andrea, upesi akageuka na kuniangalia moja kwa moja katika umati huo wote. Hapana shaka Yeye alijua ya kwamba nilikuwa na kiu.” Mungu kwa kawaida huwajia wale wanaoona kiu, na kwa kweli wanataka kumshika, kwa shauku kubwa.

⁵⁵ “Na hapana shaka aliniangalia, aliponiangalia, akasema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Hilo lilitosha kwangu mimi, kwa kuwa nilijua ya kwamba baba yangu aliniambia ya kwamba Maandiko yalisema ya kwamba Masihi angekuwa ni Nabii, naye Mtu huyu hakunijua tu kwa jina, Ambaye hakuwa ameniona kamwe, bali alimjua baba yangu pia, akaniambia nilikuwa mwana wa Yona. Hilo lilitosha.”

⁵⁶ Filipo, hapana shaka aliingia sakafuni yapata wakati huo. Sasa, hawa ni wanafunzi wa Kristo Mwenyewe ambao tunaninii...wana mkutano wa ushuhuda, si ulimwengu wa nje, wale walioishi pamoja Naye, na kulala pamoja Naye, na kuishi pamoja Naye, na—na wanajua Yeye ni nini, walimsikia akizungumza na kunena.

⁵⁷ Filipo akasema, “Simoni, hilo linishawishi, pia, kwa sababu nimesoma Maandiko maishani mwangu mwote na kufundishwa Hayo, nami nilijua kama Myahudi ya kwamba tumefundishwa kuwaamini manabii wetu. Nao unabii ulisema kweli ya kwamba Masihi, Mwana wa Mungu angekuwa Nabii kama Musa. Nilipoona ishara ya nabii ikifanywa basi nilijua huyo alikuwa ni Masihi, kwa sababu ilikuwa imepita mamia ya miaka tangu tuwe na nabii,” nafikiri yapata miaka mia nne tangu Malaki, “nami nilijua ya kwamba kitu cha pili

kutokea kilikuwa ni Masihi, na Huyo alikuwa ni Yeye. Kwa hiyo, nikashuka chini ya kilima mbio kwa rafiki yangu Filipo.”

⁵⁸ Kama tulivyomchukua jana jioni na kumpata, Filipo alimwona Nathanaeli, hasa, chini ya mti akiomba, na kusema, “Njoo, umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusuifu.”

Akasema, “Laweza neno jema kutoka Nazareti?”

Akasema, “Njoo, uone. Njoo, ujionee mwenyewe.”

Basi alipozunguka kilima, akamwambia yaliyokuwa yakitukia, akisema, “Unajua Masihi atakuwa ni nabii, tunajua hilo.”

“Loo, naam,” akasema Nathanaeli, “Ninajua itakuwa ninii, Yeye atakuwa ni nabii.”

“Vema, nimemwona akifanya mambo yayo hayo. Bila shaka, najua; nimeiona, nimejaribu, nami ninajua ni kweli.”

“Vema, nitakuja tu nione, basi.”

⁵⁹ Hao wakazunguka hicho kilima. Walipofika Mbele za Bwana Yesu, Yeye alimwangalia Nathanaeli, na kusema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake,” wakati alipoingia mstarini.

Naye akasema, “Ulinijua, Rabi?” *Mwalimu*. “Hujapata kuniona maishani Mwako. Ulipataje kunijua?”

Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Sasa, hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo.

⁶⁰ Filipo akiwa ni mwanafunzi wa Biblia aliyejua ya kwamba hivyo ndivyo Masihi alivyokuwa awe, alisema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.”

⁶¹ Ndipo Yesu akasema, “Vema, kwa sababu nimekwambia hivyo, unaamini? Utaona mambo makuu kuliko haya. Kama tu utaamini kiasi hicho, utaona makubwa kuliko hayo.” Kwanza huna budi kuamini.

⁶² Sasa, na halafu hapana—hapana shaka ilikuwa ni kijana Yakobo, ama mmoja wao aliyeketi pale aliyesema, “Mnajua siku moja . . . Sote tunamjua Rebeka, huyo ni mke wa mfanyabiashara wa Yeriko, Zakayo, anaendesha shirika la kodi huko chini, anakusanya kodi. Nasi tunajua ya kwamba Dada Rebeka alikuwa ameomba kwa bidii sana ili Zakayo a—ampokee Yesu, na kumwambia mambo yote ambayo—ambayo alikuwa ameyaona, lakini rabi alikuwa amemwambia kwamba Yeye alikuwa, si kitu Kwake, kwa sababu Yeye hakutambuliwa miongoni mwa makasisi wa siku hiyo, kwa hiyo asingemkubali.

⁶³ “Kwa hiyo Zakayo, unakumbuka ushuhuda wake kwenye Kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel asubuhi ile, wakati alipoingia na kutwambia hayo kuhusu kile kilichotukia? Alisema alienda kule chini kumwona Yesu, na

kulikuwa na umati mkubwa kupita kiasi.” Na kwa *namna fulani* mahali Kristo alipo, ni ninii tu: “Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu.” Wale wote wanaoweza kuvutwa. “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu.”

⁶⁴ Naye akasema, “Zakayo aliona kwamba, yeye akiwa ni mdogo wa kimo, kama alivyoshuhudia, asingeweza kumwona Bwana, kwa hiyo akakimbia kwenye kona nyingine, akijua ni njia gani aliyokuwa akipitia mjini, naye akapanda juu ya mkuyu, naye a—akasema, ‘Sasa, nitaketi tu hapa juu ya haya, ambapo matawi mawili yanakutana.’” Hapo ni mahali pazuri pa kuketi ambapo njia mbili zinakutana, hizo ni mawazo yako na Neno la Mungu. Mahali ambapo mawazo yako na Yake yanapokutana, hapo ni mahali pazuri pa kutulia kwa dakika chache tu, kuamua utapitia njia gani kutoka hapo.

⁶⁵ “Ndipo akaketi chini, akasema, ‘Ninakumbuka ya kwamba mke wangu aliniambia kuhusu huyu hapa Mgalilaya kwamba ni nabii. Sasa, kama Yeye ni nabii, nitamwamini, kwa sababu ninajua ya kwamba Biblia yetu ilisema, ‘Akiwepo mtu miongoni mwenu ambaye ni... aliye nabii, nami Bwana nitajifunua Mwenyewe kwake, na yale asemayo yakitimia basi msikieni, niko pamoja naye, lakini yasipotimia, basi msimsikie.’”

⁶⁶ “Kwa hiyo ni—ninajua, tena siamini, kama vile rabi wangu alivyoniambia, ya kwamba mtu aliyezaliwa maskini kama Yeye, na mwenye jina kama alilo nalo, wala hakulelewa awe rabi... Na mambo haya yote ya kimbinguni anayonena habari zake, si—siyaamini. Kwa hiyo nita—nitangojea, na nitakapomwona, nitamwambia ukweli wa mambo.’

⁶⁷ “Kwa hiyo alipoanza kuwazia juu ya yale Rebeka aliyomwambia, ‘Vema, labda Yeye ni nabii, lakini kama ndivyo alivyo, nitapata tu maoni yangu, ndipo nitarudi na kumwambia Rebeka, maana wako wengi mno.’

⁶⁸ “Kwa hiyo akapanda kwenye matawi akavuta majani yote kwake, akajifunika asiweze kuonekana, akajificha. Ndipo baada ya kitambo kidogo akasikia kelele zikija kwenye kona.” Kuna kitu cha kushangaza, mahali Yesu alipo kwa kawaida kuna kelele za namna fulani, sijui ni kwa nini, bali ndivyo ilivyo daima. Kama tu vile Haruni akiingia pamoja na komamanga na kengele, asipopiga kelele nyingi, mbona, hawakujua alikuwa hai. Nami nafikiri hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, limekufa sana hata hatusikii chochote tena; kwa hiyo, palipo na uhai, pana kelele.

⁶⁹ “Sasa, nasi tunaona ya kwamba alisema basi, wakati Yesu alipopiga kona, naye akamwangalia, alikuwa amejificha kidogo, kusudi Yesu asiweze kumwona. Kwa hiyo, alikuwa na jani, naye akashusha tu jani hili na kuangalia nje, maana hakutaka, kumwona, mfanyabiashara wa mjini, ameketi juu ya mti, hiyo kwa namna fulani ingekuwa ni aibu, mwajua. Naye

huyu Mtakatifu anayejifingirisha akiingia, kwa vyovyote vile, mwajua, akiwa na jina alilokuwa nalo, hilo lingeathiri biashara yake ka—kama wangemwona akijihusisha na Jamaa kama huyo.

⁷⁰ “Na kwa hiyo, lakini alitaka kujua kile ambacho Rebeka alikuwa akizungumzia, kwa hiyo akaketi pale, akainua jani lake juu, na kusema, ‘Ninasikia kelele, kwa hiyo labda baada ya kitambo kidogo Yeye atakuja.’

⁷¹ “Akasikia kelele naye akatazama kwenye kona, wakaja wale wavuvi wakubwa mno, wanene, wakisema, ‘Jamani, samahani, Ndugu ye—yetu amechoka sana. Yu—Yuko—Yuko njiani akitoka sasa, hana budi kwenda Yerusalemu, akasema. Je, nyote mwaweza kusimama tu kando, na kumpisha atoke nje?’ Sana, kwa diplomasia nyingi na wema.

“Wanafunzi wengine wakifuata, wakisema, ‘Jamani, laiti tungalikuwa na wakati, lakini hatuna kabisa.’

⁷² “Na, baada ya kitambo kidogo, alipopiga kona, basi Zakayo akashusha jani lake na kuanza kuchungulia, akamwona Yeye akija namna *hiyo*.” Nanyi mwajua, siamini ya kwamba mtu yeyote angeweza kumwagalia Kristo moja kwa moja na kujisikia vile vile tena, si—siamini angeweza.

⁷³ “*Kitu fulani* kikaanza kumgusa. Na kusema, ‘Mnajua nini, ni—nilininii tu, labda Rebeka alikuwa sahihi, bali nitamwagalia vizuri, kisha nitamsikia wakati mwingine, kwa sababu Yeye hanijui, mimi ni mfanyabiashara hapa, ndiyo kwanza aingie mjini, kwa hiyo Yeye hanijui, hajui lolote kunihusu mimi, wala Yeye hajui hali yangu, kwa hiyo nitaketi tu hapa juu ya mti.’

⁷⁴ “Naye akaja, ndipo alipovuka njia ya kando, akashuka, akafika moja kwa moja chini ya huo mti, akasimama na kuangalia juu, kasema, ‘Zakayo, shuka, ninaenda nyumbani pamoja nawe, leo, kwa chakula cha kutwa.’

⁷⁵ “Loo, mnakumbuka?” akasema Yakobo. “Hilo lilitosha kwangu, nilijua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake, maana tulikuwa ndio kwanza tuingie mjini. Alijuaje alikuwa juu ya mti? Na alijuaje jina lake lilikuwa ni Zakayo, na yote kumhusu? Hilo lilitosha kwangu, kwa sababu Biblia ilisema ya kwamba Yeye angekuwa ni nabii.”

⁷⁶ “Vema,” ndipo mwingine akanena, na kusema, “vipi kuhusu Bartimayo kipofu tulipotoka nje ya mji? Wakati huyo hapo ameketi huko nje akiota juu ya zile siku, akasema, alipokuwa anaona, jinsi mama yake alivyokuwa amemwambia kuhusu ile siku kuu ambayo Yehova alinena wakati mmoja kwa ajili ya watu, lakini alikuwa kipofu miaka hii yote.

⁷⁷ “Na jinsi tulipotoka nje ya mji, watu wakimdhihaki, na makuhani wakipiga makelele, ‘Wewe uliyewafufua wafu, tuna makaburi yaliyojaa hao hapa juu, njoo ukawafufue!’”

⁷⁸ Mnaona Mungu hawafanyii watu vitimbi. Yesu hufanya tu jinsi Baba anavyomwonyesha, Naye alisema hayo tu ndiyo Yeye afanyayo, Yohana Mtakatifu 5. Mnajua, wangali wana hao pepo wachafu ulimwenguni siku hizi, hata hivyo, watasema, “Hebu nimwone akimponya *huyu*. Hebu nimwone akimponya *huyo*.” Mnaona? Huyo ni roho yule yule mchafu; ni kwamba tu hawajui.

⁷⁹ Yeye yule aliyeketi pale msalabani, ama, kabla hajafika msalabani, wakati alipojaribiwa, alisema pale juu, kasema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, fanya mwujiza hapa mbele zangu, kisha uyageuze mawe haya yawe mikate upate kula, nami nitakuamini.” Mnaona?

⁸⁰ Yesu akasema, “Lakini imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate pekee.” Hakumfanyia Shetani vitimbi.

⁸¹ Basi walipomweka uani, wakaweka kitambaa usoni Mwake, wakakizungushia machoni Mwake, kisha akachukua fimbo na kugonga kichwa Chake cha thamani, kasema, “Kama wewe ni nabii, sasa, na unaweza kutwambia, kama wewe ndiye yule Masihi-Nabii, hebu utwambie ni nani aliyekupiga kichwani,” Yeye kamwe hakusema Neno. Yeye...Nguvu na karama za Mungu si za kujionyeshwa, ni za kumtumikia Mungu kwazo. Hizo ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu kufanya jambo la kumsaidia mtu fulani, sio kujitokeza kwa kiburi, na kusema, “*Mimi*, ninii yangu kuu!” Hilo silo. Mtu anapofanya hivyo, yeye ni duni machoni pang'u. Ni nani mkuu? Mmoja: Mungu.

⁸² Ndipo huenda ilikuwa, basi, mara baada ya hayo, kwamba huenda Andrea alisema hivi: “Lakini ndugu, mnakumbuka wakati alipotutuma mjini? Yeye alitwambia asubuhi hiyo alikuwa akishuka kwenda Yeriko, lakini alikuwa na haja ya kupitia Yerus-..., ama, kupitia Samaria kutoka Yerusalemu, kwenda kuzunguka Samaria halafu aende Yeriko. Mnakumbuka jinsi alivyokuwa amechoka? Na siku nzima, tulisema, ‘Mbona—mbona usile chakula? Mbona *usifanye?*’

⁸³ “Akasema, ‘Nitangojea hapa, nanyi mwingie mkajinunulie chakula.’ Sasa, tulipokuwa tumeondoka, kisha tukanunua chakula turudi, mnakumbuka tulikuja huko, nasi tukaona tulipokuwa tumefika pale, kulikuwa na mwanamke akienda zake, naye Huyo hapo peke yake pamoja na mwa—mwanamke mwenye hali mba—mbaya?”

⁸⁴ Alikuwa ni mwanamke mchafu, mwanamke ambaye tungemwita siku hizi, *wa mtaani*, mwanamke kahaba. Alikuwa, ndoa zake zilikuwa zimevurugika kabisa, naye alikuwa akiishi na wanaume bila kuolewa nao, mtu mchafu sana. Siku hizo walivaa vazi, iliwabidi kuthibitisha hilo. “Kwa hiyo tulipoona, tukija, mnakumbuka tulinyemelea nyuma ya kichaka kile, ukuta huo mdogo, tupate kuona kile Yeye angesema? Hilo ndilo lililomtatulia kila mmoja wetu.

⁸⁵ “Alimwomba huyo mwanamke ampe maji, naye akasema, ‘Tuna ubaguzi hapa. Sisi—sisi hatuninii, si kawaida kwenu Wayahudi kutuomba sisi wanawake Wasamaria kitu kama hicho.’

⁸⁶ “Yeye alisema, ‘Kama ungaliujua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe, nikupe Maji ambayo huji hapa kuyateka.’ Mnakumbuka jinsi hayo mazungumzo yalivyoendelea?”

⁸⁷ Alikuwa akifanya nini? Baba, Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, hebu sikilizeni hili, ndugu, dada: Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kamwe hakujitwalia sifa kwa kumponya mtu yeyote, Yeye alisema, “Si Mimi nizatendaye hizo kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu, Yeye huzifanya hizo kazi.”

⁸⁸ Basi angalieni yaliyotukia. Katika Yohana Mtakatifu 5:19 Yeye alisema hivi; alikuwa ameenda kwenye birika la Bethesda, kulikuwako na umati mkubwa wa watu, watu wengi zaidi kuliko walio mahali hapa usiku wa leo, viwete, vipofu, walemavu, waliopooza, viwete. Sasa, Maandiko yanasema hivyo, viwete, walemavu, vipofu, waliopooza, naye Huyu hapa anakuja! Siku chache tu kabla ya hapo, mwanamke mmoja alikuwa amegusa vazi Lake na akawa mzima. Huyu hapa anakuja, mavazi yaliyojaa nguvu, akitembea, akapita karibu na mama aliye na mtoto mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji, akapita karibu na kipofu.

⁸⁹ Na kama uliwahi kuchukua historia yake, Malaika alishuka na kuyatibua hayo maji. Mnajua maji yaliyotibuliwa ni nini, mkondo ukielekea upande mmoja, na upepo ukivuma kwa njia nyingine, ni maji hatari. Nao waliamini ilikuwa ni Malaika, na yeyote yule aliyeingia majini, akiwa na imani ya kutosha, alikomesha huo mtiririko wa maji, nao wakaponywa ugonjwa waliokuwa nao. Nao walilala huko umati mkubwa. Wengi wao hawakuamini hilo, bali wale walioliamini, ilikuwa ni uponyaji kwao. Mungu daima amekuwa na njia ya kuwaponya watu Wake.

⁹⁰ Ili wale wanaoingia kwanza, nami nimesoma vitabu juu yake ambapo walisema ya kwamba hata wangedungana visu, wakijaribu kuingia haraka wapate kuingia mle kwanza, maana mara ya kwanza alipoingia akiwa na imani ya kutosha kuvuta nguvu za Malaika, basi hakurudi labda kwa mwezi mmoja ama miwili, msimu mwingine. Nao walikaa pale daima wakingojea. Ni subira iliyoje!

⁹¹ Naye Yesu akapita moja kwa moja karibu na vipofu, viziwi, viwete, walemavu, waliopooza, kamwe hakusema kitu, mpaka alipomfikia mtu aliyelala kwenye godoro. Ni wangapi wenu ninyi Wakalifornia mnaojua godoro ni nini? Vema, mlitoka sehemu gani ya Kentucky? Nililelewa kwenye moja. Kuweka tu kitu fulani sakafuni, na kulala chini.

⁹² Akiwa amelalia godoro, huenda alikuwa na ugonjwa wa tezi dume, huenda alikuwa—huenda alikuwa na TB. Chochote kile, alikuwa nao kwa muda wa miaka thelathini na minane, ulikuwa umedumaa, haungemwua, angeweza kutembea. Yesu akijua, angalia, Yesu akijua ya kwamba alikuwa katika hali hii wakati huu wote, alisema, “Wataka kuwa mzima?” Kwa nini isiwe huyo kipofu? Kwa nini isiwe huyo kiwete? Lakini mnaona, Yeye alielekezwa.

⁹³ Sasa, angalia jibu lake, naye akasema, “Sina mtu wa kuniweka majini. Ninapokuwa nikija, mtu fulani aliye katika hali nzuri kuliko mimi ananishinda mbio na kuingia mle ndani,” mnaona, “ananitangulia.” Angeweza kutembea, angeweza kwenda, bali kuna wengine kule wasingeweza kutembea. Mnaona? Ati nasi tunganisema Yeye alikuwa na huruma? Huruma ya kibinadamu sio huruma, kujua mapenzi ya Mungu, ndiko huruma. Mnaona?

Kwa hiyo akasema, “Wataka kuwa mzima?”

Akasema, “Sina mtu wa kunitia majini. Ninapokuja, mtu fulani hunitangulia.”

Akasema, “Jitwike godoro lako, uende nyumbani mwako.”

⁹⁴ Kamwe hakuuliza jambo moja zaidi, kwa kuwa Yesu alijua asingeuliza, akalichukua, akalitwika mgongoni mwake akaenda zake. Yesu aliulizwa swali juu yake. Hebu afanye jambo lile lile siku hizi, Naye ataulizwa juu ya jambo hilo.

⁹⁵ Mtu fulani atasema, “Huyu hapa maskini Ndugu *Fulani-wa-fulani*, yeye ni maskini mtu mzuri, alikuwa mfuasi wa kanisa maishani mwake mwote, akiuza penseli pembeni, mponye. Kwa nini ukampita?”

⁹⁶ Mwangalie Yesu alivyowajibwa siku ile ile walipomshika, wakamwuliza swali, Yohana Mtakatifu 5:19: “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Ni wangapi wanaojua hayo ni—ni Maandiko? Maandiko hayawezi kukosea, kwa hiyo Yesu angeweza tu kufanya yale Mungu aliyomwonyesha katika ono kufanya, na hilo lilimfanya nabii, zaidi ya nabii, Yeye alikuwa Mungu-Nabii, alikuwa Mungu wa manabii.

⁹⁷ Baadhi ya watu siku hizi wanajaribu kuondoa Ungu kutoka Kwake, ishara Yake kama Masihi ilikuwa ni ishara ya nabii, lakini ninii Yake. . . katika ukombozi Yeye alikuwa ni Mungu.

⁹⁸ Bikira Mariamu, mwanamke, bikira, hakumjua mwanamume yeyote, Roho Mtakatifu alimtia uvuli na kuumba Seli ya Damu, Seli hiyo ya Damu ilimzaa Mwana wa Mungu, Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa, Yeye alikuwa ni Mungu. Tumeokolewa, ilisema Biblia, kwa Damu ya Mungu. Damu hutoka kwa jinsia ya kiume, himoglobini hutoka kwenye jinsia ya kiume.

⁹⁹ Ninyi watu, haya hapa majira ya kuchipua hapa nje. Nilikuwa nikiangalia leo hii, ndege mdogo huko kichakani akijijengea kiota. Loo, watajifanyia kiota. Vema, maskini ndege huyo mama anaweza kuingia kwenye kiota hicho na kutaga kiota kizima cha mayai, kama hajawa pamoja na mwenziwe, hayataanguliwa. Hiyo ni kweli. Huenda akaketi juu yake na kuwa mwaminifu sana, ayageuze hayo mayai kwa uaminifu kabisa, na kufa kwa njaa, mpaka anakuwa dhaifu sana hawezi kuruka kutoka kwenye hicho kiota, iwapo hajakuwa pamoja na mwenziwe, hayataanguliwa, hayana ile seli ya damu ndani yayo. Uhai hutoka kwenye damu, uhai uko katika damu.

¹⁰⁰ Ni kama vile makanisa siku hizi, unaweza . . . tuna makanisa makubwa sana tuliopata kuwa nayo, washiriki wengi sana tuliopata kuwa nao, waliovalia vizuri sana tuliowahi kuwa nao, waliolishwa vizuri sana tuliopata kuwa nao, pesa nyingi kuliko tulizowahi kuwa nazo, maradhi mengi kuliko tuliyowahi kuwa nayo, kwa sababu tuna kutokuamini kwingi sana kuliko tulikowahi kuwa nako.

¹⁰¹ Ni ninii tu, kuna jambo moja tu la kufanya, hayo mayai yatakaa papo hapo kwenye kiota hicho na kuoza, na vivyo hivyo washiriki wa kanisa kama hawakuwa pamoja na yule Mwenzi, Yesu Kristo, ni wakati wa kusafisha kiota, na kumrudisha mle ndani mtu mwenye imani na aliyejazwa na Roho Mtakatifu, aliye na imani iliyo hai katika Mungu aliye hai, amekuwa pamoja na yule Mwenzi, Kristo Yesu, kitu ambacho kitaanguliwa, kitu ambacho kitaleta Uzima. Hakika.

¹⁰² Yesu angeweza tu kufanya, Yeye alisema, na Maandiko hayawezi kukosea, Yeye alisema, “Sifanyi neno kwa nafsi Yangu mpaka nimwone Baba analitenda kwanza.” Sasa, Yeye alisema aliliona, *kuona*. “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile *amwonalo* Baba . . .” Rejeeni kwenye *Kamusi Simulizi*, mwone kama neno hilo si sahihi, *mwone*. Liangalieni, hata kwenye toleo la Douay, matoleo yote yanalitoa vivyo hivyo: “Mpaka *nimwone* Baba analitenda. Baba hufanya kazi, yale Baba afanyayo, Yeye hunionyesha Mimi, nami ninaenda tu na kuyatekeleza kwa ajili Yake.”

¹⁰³ Hivyo ndivyo kila nabii wa Biblia alivyofanya, ilikuwa ni kuona kwa ono jambo la kufanya, na hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi katika siku hiyo. Na kama hiyo ndiyo ishara ya Masihi katika siku hiyo, katika kumalizika kwa kipindi cha wakati wa Kiyahudi, Naye aliahidi angefanya jambo lile lile katika siku za mwisho, wakati wa kuliona likiinuka umewadia.

¹⁰⁴ Tuko katika siku ya mwisho, ulimwengu uko katika hali ya fadhaa kali, uko tayari kulipuliwa vipande-vipande, ninii, kwa sababu wamekataa, wamekana, naye Roho Mtakatifu ameijeruhi mioyo yao, na Mungu . . .

¹⁰⁵ Kama vile ma—mama mmoja katika duka la mali rahisi, hapa majuma machache yaliyopita, huko Louisville, Kentucky, alikuwa na mvulana mdogo, alikuwa akizunguka, akimwonyesha vitu, akisema, “Angalia, Mpenzi, angalia, Mpenzi, angalia, Mpenzi,” naye maskini mvulana huyo ameketi tu na kukodoa macho. Naye, baada ya kitambo kidogo, akaanguka tu kwenye kaunta na kuanza kupiga mayowe.

Ndipo baadhi ya watu katika hilo duka la mali rahisi wakamwendea, na kusema, “Kuna nini?”

¹⁰⁶ Akasema, “Ni maskini mvulana wangu.” Akasema, “Haiwezekani! Dakitari alisema amepata nafuu, lakini siyvo.” Kasema, “Miezi michache iliyopita, maskini jamaa huyo alianza tu kukodoa macho,” na kusema, “Siwezi kuvutia usikivu wake kwa chochote.” Kasema, “Kila kitu ambacho m—mvulana mdogo wa umri wake anapaswa kuangalia,” kasema, “Nitakitikisa mbele zake, naye ataketi tu na kukodoa macho.”

¹⁰⁷ Mnajua kanisa, kanisa la Kipentekoste, kwa namna fulani limefikia vile vile kwa namna fulani, Mungu alitikisa kila kitu katika Biblia mbele yao, nao wangali wameketi tu na kukodoa macho. Kuna kasoro! Ni wakati wa kuinuka, na kuamka, na kumwita Mungu. Kumbukeni, Mungu alitabiri katika Biblia Yake ya kwamba huu ungekuwa ni Wakati wa Kanisa la Laodikia wakati mambo yangetukia hivi. Sasa hebu na tumwamini Yeye.

¹⁰⁸ Wakati Andrea akiendelea na hadithi hiyo, kwa dakika moja ama mbili zaidi, Andrea alisema, “Mnajua Yeye alimwambia yule mwanamke...” Sasa, yeye alikuwa ni Msamaria. Kuna ninii tu, kama nilivyosema jana usiku, kuna jamii tatu tu za watu duniani: watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Kama tunaamini Biblia, wote walitokana na hao wawili, hao wana watatu, hao ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

¹⁰⁹ Mnakumbuka Petro alipewa funguo za Ufalme? Yeye aliufungulia wapi? Huko Pentekoste, kwa Wayahudi; akashuka kwenda Samaria, ingawa Filipo alikuwa ameshuka akaenda na kuwahubiria ubatizo wa Roho Mtakatifu, na alikuwa akiwabatiza, nao walikuwa tayari kuipokea, lakini Petro alikuwa na funguo, akashuka, akawawekea mikono, wakampokea Roho Mtakatifu; ndipo kwenye nyumba ya Kornelio, Wamataifa, Matendo 10:49, tunaona ya kwamba Petro alitumwa huko juu kwa ono, “Basi alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia.” Tangu wakati huo na kuendelea Roho Mtakatifu alikuwa tu, “Kwa yeyote atakaye, na aje,” bali alikuwa na funguo za Ufalme.

¹¹⁰ Sasa, angalieni hizo jamii tatu... Sasa, kama nilivyosema jana jioni... Ilinibidi kuharakisha, sababu ya mimi kurudia hili kwa njia nyingine, usiku wa leo. Ilinibidi kuharakisha, mlikuwa na wasiwasi, na—nao walikuwa wakisema kuna tahadhari, na

kadhalika. Sasa, kwa kuwa mumetulia zaidi usiku wa leo, na ni wanyamavu, angalieni, Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi, naye Masihi alipaswa kuja na kujitangaza Mwenyewe kwa . . . kuwa ndiye Masihi.

¹¹¹ Sasa, mnafikiri Yesu alikuja kinyume na Maandiko? Asingekuwa ni Yesu, asingekuwa Mwana wa Mungu; ilibidi aje kulingana na Maandiko, bali si kulingana na mawazo ya makanisa ya siku hizo. Alikuwa tofauti na mawazo ya kanisa, fundisho lao kulihusu, bali alikuja kulingana na jinsi Maandiko yalivyoandikwa. Na hilo ndilo ninalojaribu kuwakumbusha, usiku wa leo, jambo lile lile, anakuja kulingana na njia aliyoahidi kuja.

¹¹² Sasa, kumbukeni, kama Mungu akipata kuitwa jukwaani kutenda kazi, basi jinsi anavyotenda kwanza, hana budi kutenda kila wakati, baadaye, vivyo hivyo, la sivyo alikosea alipotenda kwanza. Kwa hiyo kama hiyo ilikuwa ndiyo njia ya kujitambulisha Mwenyewe katika siku hiyo kwa Wayahudi, na kwa Wasamaria waliokuwa wakimtazamia Masihi . . .

¹¹³ Hakuna Mmataifa aliyekuwa akimtazamia Masihi, tulikuwa Warumi na Wayunani, huku tukiabudu miungu ya chuma, felesi, marumaru, kama vile wengi wao wangali wanafanya, na—na namna hiyo, tukiwa na rungu mgongoni mwetu. Lakini sasa, baada ya miaka elfu mbili ya theolojia na mafundisho, sasa Kanisa la Mataifa, Kanisa teule, linamtazamia Masihi. Sasa, itambidi kutenda wakati atakapokuja wakati huu, kama tu alivyofanya wakati huo, itambidi kufanya mambo yale yale, maana Neno lilisema angefanya.

¹¹⁴ Sasa, ili mpate kuona ya kwamba Kristo wetu hajafa, Yeye yu pamoja nasi, akiishi ndani yetu, papa hapa pamoja nasi sasa, na sasa kama ninaweza kuwafanya muone jambo hilo, basi ni jambo rahisi sana kwenu kukubali uponyaji wenu, si kuhusu mikono yangu kuwekwa juu yako, mimi ni mwanadamu, ni mikono Yake, mtafute.

¹¹⁵ Sasa angalieni, waliposikiliza na kusikia mazungumzo ya jambo hili (Sasa, huyu ni mwa—mwanamke mwenye sifa mbaya sasa, huko Samaria. Alikuwa ni mwanamke mbaya, kwa hiyo walikuwa wakisikiliza.), nao waliposikia, Yeye alisema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.” Sasa, Yeye alizungumza naye muda mrefu kutosha kuishika roho yake. Akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

¹¹⁶ “Nanyi mnakumbuka, ndugu,” huenda Andrea aliwaambia hao ndugu wengine, kasema, “mnakumbuka jinsi sisi sote tulivyowazia, ‘Uh-loo, uh-loo, huu hapa wakati mmoja Yeye ameshikwa?’ Kwa sababu Yeye anamwambia huyo mwanamke ya kwamba hana—kwamba hana mu—mume, kasema, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa,’ hasa, kasema, ‘Nenda,

kamwite mumeo,' Yeye anamwambia yeye ana mume, naye anasema hana mume, alikuwa akilipinga Neno Lake. Sasa itakuwaje?

117 "Mnakumbuka jinsi sisi sote tulivyosimama huku masikio yetu yamechomwa, na—na baridi ikipitia juu yetu? Kuna nini? Tulishangaa: 'Je, Bwana wetu alikuwa amenaswa katika mtego? Sasa Yeye anamwambia yule mwanamke ana mume, naye anasema, "Sina mume."'

118 "Mnakumbuka jinsi tulivyowazia? Basi Yeye alininii...? Mpole tu alivyoweza kuwa, kasema, 'Umesema vema, kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.' Hayo mandhari yakabadilika upesi sana.

119 "Basi mwanamke huyu alimwambia nini? 'Bwana, mimi ni mwanamke Msamaria. Huenda ninaishi katika dhambi,'" nimefanya kitu kidogo kama hiki, "'bali nayajua Maandiko, nilitoka kwenye nyumba iliyofundisha Biblia. Mimi...Huna budi kuwa ni nabii. Ninajua, tumefundishwa, Samaria yote imefundishwa kwamba kuna Masihi ajaye, Ambaye Ji-... Ambaye atakuwa Kristo,'" maana yake ni *Mtiwa Mafuta*, "'na atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya, hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi. Huna budi kuwa nabii Wake.'

120 "Yesu akasema, 'Mimi Ndiye.'" Kamwe hapajakuwapo na Mtu ambaye angeweza kusema hivyo ila Yeye, hiyo ni kweli, ama kamwe hatakuwako. "'Mimi Ndiye.'

121 "Basi akaacha mtungi wake wa maji akakimbilia mjini, na kusema, 'Njoni, mwone Mtu,' akawaambia watu mtaani, 'njoni, mwone Mtu aliyeniambia yale niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?'"

122 Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, ni yeye yule leo, hana budi kuwa.

123 "Naam, tulikumbuka hilo, jinsi ambavyo huyo mwanamke alisema hivyo."

124 Na jinsi ambavyo Biblia ilisema ya kwamba mji wote ulimwamini Yeye kuwa ndiye Masihi, kwa sababu mwanamke huyo aliwaambia watu mjini ya kwamba Yeye, hawakuwa wamekutana hapo kabla, katika mazungumzo Yeye alisema, "Nenda kamwite mumeo."

125 Naye akasema, "'Sina.' Akasema, 'Una watano.' Nanyi watu mnajua ya kwamba hayo ndiyo maisha ambayo nimeishi, na hilo lilinishawishi ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, kwa sababu Yeye alijua siri ya moyo wangu."

126 Sasa sikilizeni, hivi Biblia haisemi hivyo, ya kwamba "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu"?"

¹²⁷ Sasa, kwenu ninyi wasomaji wa Biblia: Hivi Kitabu cha Waebrania hakitwambii, mlango wa 4, kwamba “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, tena lachoma hata kugawanya mafuta ya mfupa, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo?”

¹²⁸ Neno, na wakati Neno lililo hai, ambalo ni Kristo, linapokuja miongoni mwetu, si Hilo—Hilo lingali ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo? Neno lililo hai, Kristo, Neno lililo hai, Yeye ni Neno, Naye ni Neno lililo hai, *Hili* ni Neno herufi, na wakati Neno herufi linapoletwa pamoja na Neno lililo hai, Hilo ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo.

¹²⁹ Yesu aliwaangalia wasikilizaji Wake na kuyatambua mawazo yao. Baadhi yao walisimama hapo karibu na kusema, “Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni Beelzebuli, ibilisi.”

¹³⁰ Yesu akasema, “Ninawasamehe hilo,” kumwita Roho wa Mungu kitu kiovu, kazi ovu, “Ninawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu yuaja, nawe ukisema neno moja dhidi Yake, hutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.”

¹³¹ Basi ni nini—ni nini kumkufuru Roho Mtakatifu? Mnaona? Kumwita Roho wa Mungu kitu kichafu, ni kukufuru, huko ndiko kukufuru. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kamwita Roho wa Mungu pepo mchafu. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

¹³² Kwa hiyo, mnaona, wakati watu walipopaza sauti, na kunena kwa lugha, na kadhalika, nalo taifa hili daima limewaita kundi la watakatifu wanaojifingirisha, na wazushi, na chochote kile, mnaona ni kwa nini liko tayari kwa hukumu?

¹³³ Sasa, Biblia inasema, sasa kwenu ninyi Wapentekoste, Biblia inasema, “Kama una karama ya kunena kwa lugha, basi mtu asiye na elimu akiingia, na—na muda si muda wajua wote wananena kwa lugha, watasema, ‘Ninyi nyote mna wazimu.’ Lakini akiwepo mmoja miongoni mwenu ambaye ni nabii atakayezipua siri za moyo, basi wataanguka chini, na kusema, ‘Hakika, Mungu yu pamoja nanyi.’”

¹³⁴ Vema, kama mnaamini katika kunena kwa lugha, hivi hamjui mwendeleo wake ni nini? Hivi hamjui baraka ya juu zaidi ni nini? Hivi hamwoni Roho Mtakatifu? Ni kitu gani kinachokufanya unene kwa lugha? Unafanya hivyo mwenyewe? La, bwana. Roho Mtakatifu hufanya hivyo kama wewe ni mwaminifu. Hiyo ni kweli? Roho Mtakatifu anafanya. Hicho ndicho kitu kile kile kilichowekwa kanisani, kwanza, mitume, manabii, waalimu, wachungaji, na wainjilisti. Ni Roho Mtakatifu, Kristo aliye hai, hajafa bali yu hai milele.

¹³⁵ Wana picha Yake hapa chini mahali ilipokuwa, ilipopigiwa. Ilipigwa hapa California hapa, hivi majuzi. Ikapigwa, George J. Lacy, FBI waliichunguza, na kadhalika, mmeiona na kila

kitu, Nguzo ya Moto. Nguzo ile ile ya Moto ilipigwa picha huko Ujerumani, Uswisi, kote ulimwenguni, ambako imepigwa.

¹³⁶ Sasa, ni kitu gani? Kama hiyo. . . Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu Kristo alikuwa ile Nguzo ya Moto? Vema, wakati alipokuwa, Yohana Mtakatifu 6, alipokuwa akihojiwa, Yeye alisema kuhusu, Yeye alisema, Ibrahimu, kuhusu siku zake.

Akasema, “Vema sasa,” kasema “unamaanisha kwamba umemwona Ibrahimu, nawe ni mtu hujapata bado miaka hamsini?”

Akasema, “Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.”

¹³⁷ Basi Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto, yule Malaika wa Agano. Kwa maneno mengine, ile Logos iliyotoka kwa Mungu, alikuwa ni Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani. Na hiyo Nguzo ya Moto, ile Logos ilifanyika mwili ikakaa miongoni mwetu. Naye akasema, “Nilitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.

¹³⁸ Kisha baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Sauli, Yeye alikutana na Sauli njiani akienda zake Dameski, ndipo akamwangusha chini kwa Nuru. Hakuna mmoja wa hao wengine aliyeiona, bali Sauli aliiona. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . alitoka nyikani, akiwaleta wana wa Israeli kisha akaja akakaa ndani ya Mwanadamu, Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, na kufanya ishara za namna hii kama Masihi.

¹³⁹ Na kama Nguzo iyo hiyo ya Moto, Yesu yuyo huyo, Roho yuyo huyo akirudi ndani ya Kanisa Lake, la ulimwenguni kote, hivi si atafanya jambo lile lile? “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena,” Yeye alisema, “bado, ninyi mtaniona kwa kuwa *Mimi*, *Mimi* nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹⁴⁰ Mnaona kile ninachotaribu kufanya, enyi marafiki? Ni kuwafanya mjue ya kwamba Yesu aliyetoa ahadi katika Biblia yuko papa hapa pamoja nanyi, papa hapa sasa.

¹⁴¹ Sasa, kama ungemwendea, Naye alikuwa amevaa suti hii aliyonipa, Naye angesema . . . ungesema, “Yesu, utaniponya?”

¹⁴² Unajua kile Yeye angekwambia? “Vema, mwanangu, nilifanya hivyo.” Hawezi kufanya hivyo tena. Kama umekombolewa kutoka kwenye duka la rehani, unawezaje kukombolewa mara ya pili? Alikutoa, “*Alijeruhiwa* kwa makosa yako, na kwa kupigwa Kwake wewe *uliponywa*.” Mnaona ninalomaanisha? Uponyaji wako tayari umekamilika, wokovu wako umekamilika, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuupokea tu.

¹⁴³ Inaleta tofauti gani ni nani anayekuwekea mikono, ni kitu nani kinachofanya *hiki*, *kile*, au *kinginecho*? Popote ulipo, amini

tu, hivyo tu, lipokee. Ni, Mungu hana budi kukupa wewe. Hiyo ndiyo sababu sichukui muda mwingi sana. Wamarekani wanafundishwa desturi ya kale ya Kiyahudi ya kuwekea mikono, ambayo ni sawa, bali hiyo haikuwa ni njia ya Mataifa.

¹⁴⁴ “Vema,” Yairo alisema, “njoo, uweke mkono Wako juu ya binti yangu, naye ataishi,” Myahudi.

¹⁴⁵ Lakini yule Mrumi alisema, “Mimi sistahili Wewe uje chini ya paa langu, nena tu Neno.” Mnaona? Akasema, “Mimi ni mtu niliye chini ya mamlaka, namwambia mtu huyu, ‘Njoo,’ anakuja; na yule, ‘Nenda,’ anaenda.” Alijua ya kwamba kila kitu chini yake, yeye alikuwa akida, karne ya watu, ambalo linamaanisha “mia moja,” ambapo watu mia moja walikuwa chini yake, yale aliyosema, iliwabidi kufanya. Alitambua nini katika Yesu Kristo? Kwamba magonjwa yote na maradhi yalikuwa chini Yake, chini ya mamlaka Yake. “Nena tu Neno.” Amina. Haya basi, huhitaji kuwekewa mikono.

¹⁴⁶ Naye Yesu alisema nini? Aligeuka, akasema, “Sijapata imani kama hii katika Israeli.” Vema, hiyo ndiyo aina ya imani tunayotaka hapa California, imani ya aina hiyo, “Nena Neno.” Hilo tu ndilo linalohitaji.

¹⁴⁷ Si mtu fulani kusema, “Vema, Mungu atukuzwe, Ndugu *Nanii* aliniwekea mikono, nilihisi kitu fulani kikipitia kwangu.” Huenda ulihisi mikono yake ikiwa juu yako, lakini kamwe hukuhisi chochote. Unaona? Yesu kamwe hakusema, “Uliuhisi?” Alisema, “Uliamini?” Jambo ndilo hilo. “Kama ukiamini.” Ni ninii iliyomali-. . . Si jambo la kuhisi, ni jambo la kuamini, “Yeye aaminiye,” papo hapo ulipo.

¹⁴⁸ Sisemi kuhisi kitu, ninajua nimehisi hisia za kigeni, lakini kamwe sikuweka imani yangu juu ya hisia fulani. Siwezi kujenga Fundisho langu juu ya mhemuko, sina budi kulijenga juu ya BWANA ASEMA HIVI, kwa Neno la Mungu. Na hiyo ndiyo sababu, usiku wa leo. . . Na basi kama limejengwa juu ya Neno hilo na kuna imani ya kutosha katika hilo kulifanya Neno hilo lidhihirishwe. . . Yesu alikufa na kutoa Uhai Wake apate kulitakasa Kanisa kusudi Yeye aweze kuwa ulimwenguni kote, kote ulimwenguni, wakati wote katika Kanisa Lake, huyu Roho Mtakatifu hapa.

¹⁴⁹ Wakati Yesu alipokuwa Mungu aliyefanyika mwili, Utimilifu wa Mungu ulikuwa ndani Yake, Yeye alikuwa na Roho pasipo kipimo; tunaye kwa kipimo. Sasa, vipi kama ukitoka hapa nje uchukue kijiko kimoja cha—cha maji kutoka baharini? Vema, hayo—hayo ndiyo Yesu aliyokuwa nayo, bahari yote, bali mimi na wewe tuna kijiko kimoja, hiyo ndiyo tofauti, kamwe usingelikosa. Haimbidi Yeye kuwa nasi, bali hatuna budi kuwa Naye. Lakini kama ulichukua kijiko hicho kilichojaa maji na kukipeleka kwenye maabara, kemikali zile zile zilizomo katika bahari nzima ziko kwenye kijiko hicho.

¹⁵⁰ Na wakati Mungu, kwenye Siku ya Pentekoste, aliposhuka kama upepo unaoenda kasi, mliona? Alikuwa ni Nguzo ya Moto. Lakini mliona Yeye alijigawa Mwenyewe kutoka kwa ile Nguzo ya Moto, akajigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake, ndipo Ndimi za Moto zilizogawanyika zikakaa juu ya kila mmoja wao? Mungu akijigawa Mwenyewe kwa Kanisa Lake. Si ajabu Yeye alinena, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Ikiwa wawili watakubaliana juu ya jambo lolote, na kuomba, nitawapa.” Mnaona?

¹⁵¹ Ni kitu gani hicho? Wakati Moto mdogo *hapa* na Moto mdogo *hapa*, kila mmoja wenu ni sehemu ya Mungu, tunapokutana, ni Mwili wa Kristo ukiungana. Mungu akijigawa Mwenyewe, akinipa mimi sehemu, nawe sehemu, na sehemu kwa jamaa huyo mwingine, kusudi sote tuweze kuishi, na kuwa na Uzima wa Milele. Na sasa, huo Uzima wa Milele unatokana na neno, neno la Kiyunani, kama nilivyosema, *Zoe*, ambalo linamaanisha “Uzima wa Mungu Mwenyewe.”

¹⁵² Sasa, hapana shaka ilikuwa ni wakati walipokuwa wakishuhudia hili, mara Andrea hapana shaka aliketi chini, na hapana shaka Shetani aliangalia nyuma kupitia kwenye hayo mawingu meusi, ninafunga sasa, naye akawaona wameondoka bila Yesu. Hilo ni zuri tu kama alivyotaka.

¹⁵³ Na sasa, ndugu zangu, dada zangu, hebu na tuangalie sasa, moja kwa moja katika imani, walikuwa wameondoka bila Yesu, Ninaamini ya kwamba hilo ndilo lililotendeka kwa kanisa kufanyiza Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, kanisa limeondoka bila Yesu. Tumeenda kombo kwa hamaki kuu, tumeenda mahali ambapo tuna mradi mkubwa wa ujenzi, tuone ni nani angeweza kujenga kanisa lililo kubwa kuliko yote, tumeenda kombo kwenye miradi ya elimu, tumeenda kombo kwenye miradi ya kimadhehebu, tumeenda kombo kwenye miradi ya kila namna, nasi tumeangua nini? Tumeangua kundi la watoto wa kimadhehebu. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁴ Tunajenga—tunajenga mambo ye—ye—yetu juu ya dhehebu *letu*: “Usishirikiane *nao kule*, usiwe na *hili hapa*, *sisi* ndio dhehebu, *tuna* kweli *yote*.”

¹⁵⁵ Kumbuka, ndugu, blanketi inaenea kila mahali, unaona, inamfunika huyo jamaa mwingine, pia. Unaona? Lakini tumejiwekea mipaka na kujitenga wenyewe, kama tu vile Wabaptisti, Wamethodisti, na hao wengine walivyofanya. Walikuwa wakizungumza juu ya Wabaptisti baridi, wa kawaida, sasa ni Wapentekoste baridi, wa kawaida. Mnaona? Wabaptisti wanajipasha moto.

¹⁵⁶ Angalieni jinsi...Sasa, ni kweli. Tuliangua watoto wa kimadhehebu, tumewaangua watoto wa kielimu; tumefanya shule za Biblia, sawa kabisa, lakini imetubidi kuwaambia nini? “Wapeni Shahada ya Sanaa, na Ph.D., na LL.D.”

¹⁵⁷ Na hata baadhi ya madhehebu yetu makuu, kabla hawajamtuma mmishenari, Pentekoste sasa, kabla hawajamtuma mmishenari wa Kipentekoste ng'ambo, hana budi kuchunguzwa na tabibu wa magonjwa ya akili kuona kama IQ yake ni kubwa vya kutosha. Hilo ni doa kwenye jina la Pentekoste! Pentekoste si dhehebu, Pentekoste ni tukio ambalo watu wote wanaweza kuwa nalo, Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, ama *wowote wale*.

¹⁵⁸ Ni nani atakayeamua kama yeye ni mmishenari au la, Roho Mtakatifu, ama tabibu fulani wa kilimwengu wa magonjwa ya akili? Mungu hutoa miito. Elimu ya Petro isingalistahili hayo, Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa, bali Roho Mtakatifu, ilimpendeza Roho Mtakatifu kumfanya kiongozi wa Kanisa; yeye na Yohana, wote wawili wasio na elimu wala maarifa. Lakini hapo ndipo tulipo.

¹⁵⁹ Ibilisi alituona tukienda kwa hamaki kubwa namna hii, naye anasema, "Hii hapa nafasi yangu." Hilo ndilo jambo lile lile alilofanya kule. Kwa hiyo, alisimama juu ya milima na kuanza kupuliza pumzi yake yenye sumu, akasema, "Hao hapo, wamelundikana huko katikati ya bahari ile, wanashuhudia yale yaliyokuwako. Sasa naona hawako naye tena sasa, hayuko pamoja nao tena sasa."

¹⁶⁰ Basi angalieni Wakati wa Kanisa la Laodikia, kati ya nyakati zote za kanisa, nyakati saba za mwisho za kanisa, Laodikia, Yesu alikuwa nje ya kanisa Lake Mwenyewe, akibisha, akijaribu kurudi ndani. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] Sasa, hapo ndipo tumefikia.

¹⁶¹ Na kwa hiyo Shetani amekuwa akipulizia pumzi yake ya sumu kote, mwajua, akisema, "*Whiu! Whiu!* Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho. Msiamini upuuzi kama huo, ni telepathia ya kiakili. Hiyo ni kweli." Wanaliacha Neno. Mi—mimi. . . Hebu lichunguze tu Neno uone kama si sahihi, ndipo uone kama Mungu hutoa Neno hilo na kulithibitisha, ndipo inalifanya sahihi; Mungu anaposema hivyo, hilo latosha.

¹⁶² Sasa, "Siku za miujiza zimepita," wamekuwa wa kawaida, wanazungumza tu juu ya makanisa yetu, na ninii yetu, yale tutakayofanya, na mipango yetu mikuu tuliyo nayo. Unaona, aliona hawana, ndipo hiyo meli ndogo ikaanza kuvuma na kurukaruka, nasi tunaona kwamba matumaini yote ya uamsho yamekwisha.

¹⁶³ Ni karibu namna hiyo leo, Mungu alimtuma Oral Roberts kote nchini, akamtuma Tommy Osborn kote nchini, Yeye—Yeye alimtuma mmoja baada ya mwingine, wimbi baada ya wimbi, baada ya wimbi, baada ya wimbi, nasi hawa hapa tungali tumeketi bila uamsho. Kuna nini?

¹⁶⁴ Lakini kumbukeni, Yeye hakuwa amefika mbali sana, wakati alipowaona wakienda kombo, alijua lililokuwa linaenda

kutukia; na hiyo ndiyo sababu Yeye alijua hapa, angeweza kubashiri mwisho hapo mwanzoni. Alijua Wakati wa Kanisa la Laodikia ulikuwa unaenda kumsukuma nje, kwa hiyo akafanya maandalizi kukabilia na, “Wale niwapendao, ninawarudi na kuwakemea. Nimesimama mlangoni na kubisha, mtu yeyote akifungua, na kuniruhusu niingie, nitaingia na kula pamoja naye,” kama utafungua tu, umruhusu aingie.

¹⁶⁵ Na wakati pepo zinapovuma, na ni kinyume, nasi tunaona ni vigumu kusogea, hivyo ndivyo walivyokuwa, bali alikuwa amepanda kilima kirefu kuliko vyote vilivyokuwako Galilaya, mlima mrefu kuliko yote katika Palestina labda, alikuwa juu mlimani, kadiri unavyopanda juu zaidi, ndivyo unavyoweza kuona mbali, Naye akapanda kule juu kusudi aweze kuwalinda. Ndipo alipowaona katika dhiki . . . Alikuwa juu vya kutosha hata angeweza kuwaona.

¹⁶⁶ Na wakati alipokuwa hapa duniani, alitambua ya kwamba tulikuwa tunakuja kwenye hali hii, kwa hiyo Yeye hakupanda tu ule mlima wa Kalvari, bali alipanda kupita mwezi na nyota, mpaka akaketi mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, nalo jicho Lake liko juu ya shorewanda, nami ninajua Yeye anauangalia mkutano huu, usiku wa leo. Hajaenda mbali sana, anakuangalia.

¹⁶⁷ Wakati meli ndogo inaporushwa-rushwa, mvulana huyu *hapa*, maskini meli yake, yako, yako, hapa nje, kote kote, meli yako ndogo ikiyumbayumba, “Daktari anasema siwezi kupona; nimepooza; nina kansa; nitakufa,” Yeye anajua hilo, bali jicho Lake liko kwenye shorewanda, alikukomboza, alilipa gharama, “Alijeruhiwa kwa makosa yako; kwa kupigwa Kwake uliponywa.” Matayarisho yamefanywa, Naye akapanda juu kwenye ngome za Utukufu, na kuketi mkono wa kuume wa Mungu huko Juu, akikulinda, akiishi daima kufanya maombezi.

¹⁶⁸ Biblia ilisema Yeye amesimama pale, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa hapa duniani, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama ungemgusa, Yeye angetenda kama alivyotenda alipokuwa duniani, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

¹⁶⁹ Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, akatoka nje na kuingia kwenye umati, na kuketi chini. Hakuingia mstarini, hao wengine walikuwa mstarini, hakuingia mstarini, kwa hiyo aligusa vazi Lake, akaenda, akaketi kwenye kusanyiko.

Ndipo akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

Ndipo mtume Petro akamkemea, na kusema, “Kila mtu anakugusa. Kwa nini unasema jambo kama hilo?”

Akasema, “Lakini nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka,” ono. Jambo fulani lilitukia, ulikuwa ni mguso wa aina fulani.

¹⁷⁰ Mipango hii yote siku hizi haimgusi Yeye, inahitaji moyo wa mtu binafsi kumgusa, si hofu, mtu fulani atakayeamini hilo, uweke kando ushirikina wako na umwamini Yeye.

¹⁷¹ “Mtu fulani alinigusa,” Yeye akasema, “nimekuwa dhaifu, nguvu,” uweza, “zilinitoka.” Ndipo akaangalia kote juu ya kusanyiko mpaka akamwona maskini mwanamke huyo, akamwambia ugonjwa wake wa kutokwa na damu aliokuwa nao, “imani yake imekuokoa.” Mnaona? “Imani yako imeokoa.” Sozo, “imeokoa,” neno lile lile, kimwili au kiroho. Mnaona? “Imani yako imekuokoa.”

¹⁷² Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, kama ungengusa, angetendaje? Kama Yeye ni yule yule, angetenda vivyo hivyo.

¹⁷³ Ninalisai kusanyiko hili, usiku wa leo, kuamini hadithi hiyo kuwa ni kweli: Angalia kama Yeye angali si Kuhani Mkuu yeye yule, angalia kama Yeye hatendi usiku wa leo, kama alivyofanya alipokuwa Galilaya, angalia kama hatendi jambo lile lile.

¹⁷⁴ Hatuigizi kanisa, saa zimeenda sana, jua linatua, ni wakati wa kuwa na uhalisi, wakati wa wanaume na wanawake kutupa makoti ya—ya—yao ya kanisa, mweke kando matambara yenu ya kimadhehebu na kumwangelia Mungu, na muwe na uamsho wa Kipentekoste katika kanisa la Kipentekoste. Mguse uone kama Yeye angali ni Kuhani Mkuu, ninakupa changamoto hiyo, amini, uone kitakachotukia.

¹⁷⁵ Kwa hiyo akaja kwao akitembea juu ya maji, saa yao ya mwisho, matumaini yote yamekwisha. Ilikuwa? Mara walipomwona, kama tu walivyomwona wakati huo, wanafanya leo, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikiogopa, walidhani kilikuwa ni mzuka, “Yeye ni kivuli.”

¹⁷⁶ Na jambo lile lile siku hizi! Ninyi Wabaptisti, ninyi Wamethodisti, ninyi Wapresbiteri, Wakatoliki, ninyi Wapentekoste, Umoja, Utatu, Utano, Assemblies, Foursquare, chochote ulicho, ninyi ni watoto wa Mungu, bali msiope, Mungu aliahidi angefanya hivyo. Kama angeweza kunena usiku wa leo, angesema kama ilivyokuwa wakati huo, wakati wote walipoogopa. “Vema,” kasema, “tunaona kivuli fulani, kinaonekana kama mzuka, kuna kitu kigeni kwake.”

Kasema, “Msiope; Ni Mimi,” yeye yule jana, leo, na hata milele. “Msiope; Ni Mimi.”

¹⁷⁷ Hivi ninyi, enyi kanisa, usiku wa leo, hamtamwacha aingie kwenye jahazi lenu dogo mnapoabiri kwenye barabara adhimu ya maisha? Hivi hutaufungua tu moyo wako, na kusema, “Bwana Yesu, ninakuamini Wewe, ninataka, ninajua hayo ni Maandiko, huyu mtu aliniambia yaliyo Maandiko, ninajua ya kwamba Biblia inasema Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele; nayajua mambo haya?”

178 Hatuna wakati wa kuingilia yote usiku wa leo, tutaendelea nalo kesho usiku, zaidi na zaidi, mnaona, tuendelea tu, tukikuonyesha na kukuthibitishia, ewe rafiki, yale uliyoamini yamekuwa kweli, bali tunaishi mbele kidogo barabarani sasa.

179 Hiyo ndiyo shida ya Wakristo. Mnajua sayansi haichukui yale sayansi iliyosema miaka mia mbili ama mia tatu iliyopita. Ilikuwa ni mwanasayansi Mfaransa aliyesema, yapata miaka mia tatu iliyopita, akalithibitisha kwa kuzungusha mpira duniani, naye akasema, “Kama mtu yeyote angeweza kwenda mwendo wa kasi sana wa maili thelathini kwa saa,” akathibitisha kisayansi ya kwamba nguvu za uvutano zingekuondoa duniani. Vipi kuhusu Ricky na gari lake la kasi? Wanazunguka yapata maili elfu kadhaa kwa saa. Mnafikiri wanaangalia nyuma na kuona yale ambayo sayansi hiyo inasema? La. Wangali wanaendelea, wanasonga mbele.

180 Bali kanisa, watasema, “Hebu tuone kile Bw. Moody alisema juu yake. Hebu tuone yale Bw. Wesley aliyosema.” Hao watu waliishi katika wakati wao, hilo lilikuwa sawa kwa wakati huo, bali hatuna tu mti wa kisayansi wa kupanda, tuna rasilimali zisizotumiwa bado za baraka nyingi za Mungu, ambazo hazijawekewa mpaka, bali hazina kikomo.

181 “Lolote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu nitalifanya.” Kila ahadi katika hiki Kitabu ni yako. Unapookoka, Yeye anakupua hundi iliyoandikwa Jina Lake chini yake, usiogope kuijaza, maana Benki ya Mbinguni itaitambua kama itapitia kwenye nyumba ya kulipia ya Kipentekoste. Kwa hiyo mnaona, hiyo ni kweli. Mnaona, kama una kitu fulani pale kwenye akiba, wewe mwenyewe, unaona, kama umetambuliwa, kama una utambulisho wa kuonyesha ya kwamba hiyo hundi ni yako, ni—ni kwa ajili ya waaminio tu sasa, kama una utambulisho huo, mbona, Mungu ataitambua hundi yako. Hiyo ni kweli. Haidhuru unaomba nini, baraka zozote za ukombozi ni zako.

182 Sasa, nimezungumza nanyi kwa kirefu, nami najua viungo vyenu vinakakamaa. Ninyi wazee, na vijana, na wote, mliosimama ndani, nje, kwenye milango, Mungu awazawadie sana.

183 Mimi ni ndugu yenu. Hakuna . . . Sina hata chembe moja ya nguvu za uponyaji, hakuna mtu mwingine yeyote aliye nazo, hakuna daktari aliye na zozote, hakuna dawa iliyo na zozote. Hakuna dawa ulimwenguni ambayo itakuponya, hakuna daktari aliye na akili timamu atakayekwambia hivyo; Mayo Brothers walisema hawana dawa itakayoponya.

184 Kama nikiukata mkono wangu kwa kisu, hawana dawa ulimwenguni, itakayoponya jeraha hilo la kisu. Dawa yoyote itakayoponya jeraha la kisu mkononi mwangu ingeliponya kwenye dawati hili, ama kwenye koti langu. Mnasema, “Dawa

haikutengenezewa dawati lako, wala ko—koti, ilitengenezwa kwa ajili ya mwili wako.”

¹⁸⁵ Vema, vipi kama nikiukata mkono wangu, nianguke nife, nawe unitie dawa nisioze na kunifanya nionekane wa kawaida kwa miaka hamsini, unidunge sindano ya penisilini kila siku, na kila namna ya marhamu, kisha unishone, na kadhalika? Miaka hamsini tangu leo, hilo jeraha litaonekana tu kama lilivyokuwa wakati ulipokatwa. Kama inauponya mwili wa mwanadamu, kwa nini isiuponye?

Vema, unasema, “Hakika, uhai umemtoka.”

¹⁸⁶ Vema, niambieni uhai ni nini, nami nitawaambia Mungu ni Nani. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ni Mungu. Dawa haijengi tishu, inahitaji uhai kujenga tishu. Hiyo ni kweli. Na mtazamo wako kwa Mungu ndio unaofanya jambo hilo.

Mtu fulani aliniambia, “Vipi kuhusu penisilini kwa mafua makali?”

¹⁸⁷ Nikasema, “Ni kama kuwa na nyumba iliyojaa panya, nawe utie sumu ya panya, uwaue, haizibi hayo mashimo, inaua tu panya.” Hiyo ni kweli. Na hiyo ni . . . Inaua vijidudu, hiyo ni kweli, dawa huenda ikaua kijidudu, bali haijengi seli ambazo hicho kijidudu kiliharibu, hilo linahitaji Mungu kufanya hivyo, na Yeye pekee, “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote.”

¹⁸⁸ Vipi kama ulivunja mkono wako, ukaingia ndani, kasema, “Daktari, uponye mkono wangu, nataka kuzungusha mpini, ninatengeneza gari langu hapa nje, nataka kumalizia.” Angesema unahitaji uponyaji wa akili, na hiyo ingekuwa ni kweli. Huenda akaurudisha mkono wako, bali Mungu hana budi kutoa kalisi, na maada ya uhai, na kadhalika kuuponya pamoja, inahitaji Mungu. Hatuna kitu kitakachoponya, hakuna dawa inayoponya, Mungu huponya. Na mtazamo wako kwa Mungu, Yule anayeponya . . .

¹⁸⁹ Na bado hatuwezi kujua uhai ni nini. Tunajua utetelezi unaobeba uhai, bali hatujui chembechembe ya uhai ni nini, maana ni roho, wala hakuna darubini inayoweza kuona roho, haya basi. Kwa hiyo huyo Ndiye anayeponya.

¹⁹⁰ Utamwamini, usiku wa leo? Kama atakuja kwenye kusanyiko, usiku wa leo, kundi dogo tu, tutamwita mtu fulani hapa juu, nafikiri tulisambaza lundo la kadi jana usiku, moja hadi mia moja, ninaamini katika A. Tunazo chache, ilitubidi kuharakisha. Lakini, usiku wa leo, kama tu tutaita watu fulani hapa nje, na kumwacha Roho Mtakatifu aanze kutenda kazi hapa kwenye juk-. . . Kama atafanya hivyo, sisemi atafanya. Na halafu kama atatoka aingie kwenye kusanyiko na kuanza kutembea kwenye kusanyiko, na kufanya jambo lile lile huko nje, ninyi msio na kadi za maombi, kama atafanya hapa kwa

kadi za maombi, wewe gusa tu vazi Lake, uone kama Yeye si—kama Yeye si Kuhani Mkuu yeye yule.

Ni wangapi wangeamini kama mngeona yale niliyozungumzia usiku wa leo, yakitimia? Inueni mikono yenu, kote jengoni.

Sasa inamisha kichwa chako.

¹⁹¹ Baba yetu wa Mbinguni, huu ndio umbali ambao mtu yeyote angeweza kwenda, ingekuwa kulifafanua Neno. Sasa, imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno. Hapa wamelala watu kwenye vitanda vya wagonjwa, machela, viti vya magurudumu, kuna wengine huko nje wanaokufa kwa ugonjwa wa moyo, kansa. Hapana shaka ila kuna namna zote za magonjwa hapa ndani.

¹⁹² Baba Mungu, huenda kukawa na wasioamini walioketi karibu, huenda kukawa na wasioongoka walioketi karibu, kama wapo, Baba, kama wakiona Uwepo Wako ukishuka kuthibitisha ya kwamba Wewe ni—Wewe ni Mungu Yule aliyefanya ahadi miongoni mwetu, hakika, kama utafanya kiasi hicho, tutaamini hadithi ya ukombozi kwamba Wewe ulikufa kwa ajili ya makosa yetu, na kwa kupigwa Kwako sisi tuliponywa. Tujalie, Bwana.

¹⁹³ Ninajikabidhi mwenyewe, kusanyiko hili, yote mikononi mwako. Na, Baba Mungu, ninakupenda kwa ajili ya Neno Lako. Napenda wasikilizaji hawa wazuri sana ambao wamesikiliza kwa makini, wamesimama wakikakamaa, miguu yao imeshupaa na inauma. Lakini, nisikie, Bwana, tafadhali. Wakati umati huu utakapoondoka kwenye uwanja huu wa maonyesho usiku wa leo, na kuanza kurudi nyumbani kwao . . .

¹⁹⁴ Bwana, siku moja baada ya Wewe kusulubiwa na kuzikwa, walidhani yote yalikuwa yamekwisha, ulikuwa umekufa na kuzikwa na hakukuwa na lingine, kulikuwa na watu wawili, Kleopa na rafiki yake, walikuwa wakienda zao Emau, Mtu fulani alitembea pamoja nao siku nzima, akiwazungumzia kuhusu Neno la Mungu. Hawakutambua Huyu alikuwa ni Nani, lakini alipowapata usiku huo, aliwaingiza ndani ya jengo na kufunga mlango, akafanya jambo fulani mbele yao kama tu alivyofanya kabla hajasulubiwa, wakalitambua, maana hakuna mtu mwingine aliyelifanya hivyo, wakajua ya kwamba ilikuwa ni Yeye. Ndipo upesi Yeye akatoweka wasimwone, nyuma ya pazia, mahali fulani, akatoweka. Wakiwa na miguu myepesi, wenye moyo mwepesi walirudi mbio kuwaambia wanafunzi wengine, “Kweli Bwana amefufuka.”

¹⁹⁵ Hivi Wewe, usiku wa leo, utafanya jambo lile lile, Bwana? Je, utakuja miongoni mwetu na kutenda na kufanya kama tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa, kusudi kusanyiko hili lijue ya kwamba Wewe ndiwe Mungu wao na Mwokozi wao, Nawe umekuwa Ndiwe uliyewalisha na kuwabariki?

¹⁹⁶ Na jalia watambue kama Wewe utafanya jambo fulani kama ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, wajue ya kwamba Wewe hujafa, bali Wewe u hai milele, kama vile Maandiko yasemavyo Wewe ni, “Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kama utafanya hivyo, Bwana, sote tutarudi nyumbani tukisema kama walivyosema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁹⁷ Hakika, Mungu atatusaidia usiku wa leo, pamoja na kusanyiko kama hili, linalosimama kwa subira.

[Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]
(Naam.) [Ndugu huyo anaomba gari lihamishwe.]

¹⁹⁸ Asante, naam, Ndugu. Vema. Hilo ni sawa. Kama ungekuwa mwema sana. Ninamwona mtu fulani akiondoka sasa, kwa hiyo nadhani ndugu huyo atatoka vizuri. Asante.

¹⁹⁹ Niliwaweka muda mrefu sana usiku wa leo, lakini nina—ninajaribu tu kuninii... Mnaona, kama ukiruka tu ndani, bila kujua unalofanya, basi kuna faida gani? Unaona? Lakini ninyi, na—nataka kuwafikisha mahali ambapo mnaweza kuona ya kwamba ni Maandiko, ni kutimizwa kwa Maandiko. Sasa, jana usiku tulichukua somo ambapo Yeye alikuwa, Masihi alikuwa aonekane katika mwili wa waaminio katika siku hii ya mwisho kufanya na kutenda jambo lile lile alilofanya wakati huo.

²⁰⁰ Sasa, ninaamini sisi... Ni wapi ambapo...? Tuliaanza na namba moja jana usiku, tukaita baadhi, sivyo? Tuliwaita wachache tu kuanzia namba moja. Tutaendelea tu kuwaita miongoni mwao mpaka tutakapowaleta hapa juu.

²⁰¹ Hebu tuanzie, usiku wa leo, mahali pengine. Kila wakati tuliwaambia tungeninii... Niliwaambia ndugu wahudumu kwamba tungeanzia mahali fulani kila usiku, kutoka kwenye kadi zile zile, mahali fulani kila usiku.

²⁰² Hebu tuanzie, tuseme kutoka themanini. Hiyo ingekuwa themanini, na tuone kama tunaweza... Tungeweza kuwasimamisha wangapi hapa? Tungeweza kusimamisha yapata watu kumi na watano au ishirini, labda. Ni nani aliye na kadi ya maombi themanini? Inua mkono wako. Kadi ya maombi... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...nawe unataka Yesu akuponye, inua mkono wako, wote ambao hawana kadi ya maombi.

²⁰³ Vema. Sasa, wakati wao... mabawabu wanapowapanga, sasa pamoja na ninii yangu... Kumbukeni tu, kadi hiyo ya maombi haina uhusiano wowote nao. Ni wangapi wamewahi kuwa mkutanoni hapo kabla na wanajua hiyo ni kweli? Inueni mikono yenu. Hakika, haina uhusiano wowote nao, hata jambo moja.

204 Sasa, ninyi mnaoketi huko nje ambao hamna kadi ya maombi, ombeni tu, na kusema, “Ndugu Branham, haniujui. Bwana, aliniambia muda mfupi uliopita, ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Sasa, nitakugusa Wewe, ninasahau kuhusu Ndugu Branham aliyesimama pale, bali nitakugusa Wewe. Imani yangu inakutazama Wewe, Bwana, nataka kukugusa Wewe.”

205 Sasa, usiwe na wasiwasi juu yake, hakuna kitakachotukia. Kwa utulivu tu, imani tu ya kawaida, sema tu, Bwana, “Jalia nikuguse Wewe.” Na useme basi, “Ningejuaje ya kwamba Wewe...ya kwamba nilikugusa Wewe? Mfanye Ndugu Branham ageuke na kuniambia, kama tu ulivyofanya wakati yule mwanamke alipokugusa kupitia Mwanao, Yesu. Ndugu Branham na hao wahudumu hapo ni wana Wako waliopewa mamlaka,” unaona, “lakini wanachukua mahali pa Mwana wakati Yeye yuko Huko juu akifanya upatanisho kama Kuhani Mkuu.”

206 Yeye ni Ndugu yetu mkubwa. Mlijua hilo? Hakika. Na sisi ni—sisi ni watoto wa Mungu, pia, kwa kufanywa wana wenye mamlaka Naye.

207 Sasa, kama kila mtu hatasogea kwa dakika chache sasa, tulieni kabisa kwa dakika chache. Amini kwa moyo wako wote.

208 Vema. Sasa, ni wangapi humu jengoni hatufahamiani, nawe unajua ya kwamba sijui lolote kukuhusu? Inua mkono wako. Kusanyiko lote. Hakuna mtu mmoja ninayeweza kumwona katika jengo hili ninayemjua, ila nanii wangu, nilimwona rafiki yangu, Welch Evans, hapa muda mfupi uliopita kutoka Georgia ameketi hapa juu, nyuma kabisa *hapa*, ndivyo hivyo. Yeye na mke wake, na Ndugu Fred Sothmann, na, mmoja wa wadhamini wa kanisa langu kutoka Jeffersonville wameketi papa hapa nyuma mahali fulani, na Ndugu na Dada Simpson wameketi karibu naye. Hao ndio watu pekee katika jengo hili ninaowajua, nje ya Ndugu Borders, Ndugu Gene Goad, papa *hapa*, na, vema, mwanangu alikuwa hapa, bali hayupo hapa sasa. Lakini hao tu ndio ninaowajua, mnaona.

209 Sasa, sasa, kama sikujui...ninataka kuwaulizeni swali hili sasa. Tunachukua muda wetu, maana iwapo kamwe unataka kuingia hapa, jambo fulani litatukia.

210 Sasa, kama Yesu alikuwa ninii, ni yeye yule jana, leo, na hata milele, je, Biblia inasema hivyo? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye tayari amekukomboza na maradhi na—na mauti? Semeni, “Amina.” [“Amina.”] Vema, Yeye asingeweza kukukomboza tena, sivyo?

211 Sasa, kama Yeye angekuwa amesimama hapa, Mwenyewe, asingeweza kufanya jambo moja zaidi kulihusu, kuliko angeweza kuwa anaishi kupitia mimi na wewe. “Yeye

anipokeaye Mimi, anampokea Yeye aliyenipeleka. Yeye awapokeaye ninyi, anipokea Mimi.” Hiyo ni kweli? “Yeye anipokeaye mimi, anampokea Yeye aliyenipeleka.”

²¹² Sasa, kama tu utampokea Roho Mtakatifu, Ujumbe Wake . . . Sasa, nimewanukulia Biblia. Mnaona? Kuwaambia tu yale aliyofanya, na yale aliyoahidi katika mchezo mdogo wa kuigiza, kusudi watoto wadogo wataninii . . . Nafikiri maskini mtoto huyu aliyeketi *hapa*, na wengine wengi *hapo*, na maskini mtoto mchanga anayenyonya kidole gumba ameketi *pale*, ninaangalia, moyo wangu unamwonea shauku, na kila kitu mimi . . .

²¹³ Sasa, sasa, kama—kama Mungu huyu aliyeifanya Biblia, aliyeiandika Biblia . . . Unaamini Mungu alivuvia . . . Biblia imevuviwa, Neno la Mungu? Unaamini? Unaamini kwa moyo wako wote? Vema, ni Neno la Mungu lililovuviwa. Basi kama ni Neno la Mungu lililovuviwa, basi kama uvuvio wa Mungu upo hapa pamoja nasi kulifanya Neno hili liishi, kuthibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa, hakika ungeweza kumpokea. Hiyo ni kweli?

²¹⁴ Sasa, sasa, ninataka kujua, ninyi katika mstari huu wa maombi, kila mmoja wenu ambaye ni mgeni kwangu, ambaye sijui lolote kukuhusu, inua mkono wako. Unaona? Sasa, yote ni ya kigeni, kila mtu ni mgeni.

²¹⁵ Sasa kumbukeni, mimi si mponyaji, wala hakuna mtu mwingine aliye mponyaji, Mungu ndiye Mponyaji, hiyo ni kweli. Sasa, kama Yesu alikuwa amesimama hapa sasa, usiku wa leo, kama nilivyosema, amevaa suti hii aliyonipa, na kama alitaka kujitangaza Mwenyewe, ungejua kama ni Yeye? Angetenda vile vile alivyotenda alipokuwa hapa duniani. Hiyo ni kweli? Angefanya jambo lile lile, ndipo ungejua basi, Yeye alikuwa ndiye Masihi.

²¹⁶ Sasa, mimi si Masihi, hakuna mtu mwingine aliye Masihi, Yeye ndiye Masihi, bali Roho Wake anakaa ndani yetu. Mnaona? Sio sisi, maana mimi, kwa nafsi yangu . . . sasa huyu hapa mwanamke. (Huyu ndiye mwanamke wa kuombewa? Vema.)

²¹⁷ Sasa, simjui huyu mwanamke, sijawahi kumwona maishani mwangu. Aliinua mkono wake dakika chache zilizopita kwamba hatufahamiani. Huu hapa mkono wangu, Biblia ikiwa wazi hapa, simjui, sijawahi kumwona. Hunijui, sisi hapa, hatufahamiani. Sasa, sasa, hii hapa picha nzuri sana ya Yohana Mtakatifu 4, haya hapa mandhari kama kisima pale, huko nje kwenye kisima cha umma Samaria.

²¹⁸ Sasa, kila mtu humu ndani awe tayari kulipokea sasa, mnaona, ndipo hili—hili lingelitatusa papa hapa. Iweni tayari; iweni tayari; wewe, wewe, kila mahali hapa, iweni tu tayari. Mnaona? Maana kama unaweza kumwona akiingia, na kufanya vile vile hasa, hiyo inaonyesha kwamba Yeye hajafa, Yeye yu

hai hapa akiliangalia Neno Lake. Na merikebu yako ndogo imerushwa-rushwa huku na huku. Unaona? Basi amini.

219 Likubali tu, usiogope, Yeye alisema, “Ni Mimi; msiogope.” Sasa, kumbukeni hilo: “Msiogope; Ni Mimi.” Msiogope kuamini Neno Lake. Sema, “Ninakuumini Wewe, Bwana. Nitapata afya.” Fanya hivyo tu. “Msiogope; Ni Mimi.”

220 Sasa sikilizeni, kama mimi na mwanamke huyu hatufahamiani kabisa, wala hatujawahi kuonana, kama nimetiwa mafuta na Roho Mtakatifu na ningemwambia jambo fulani maishani mwake, kama Yesu alivyomwambia yule mwanamke kisimani, chochote kile kilicho maishani mwake, hatujawahi kuonana, ingebidi ije kupitia nguvu fulani za kiroho. Hiyo ni kweli? Tunajua hilo. Ingekuwa ni mwujiza. Ni wangapi wanaojua hilo? Mwujiza ni kitu, hakiwezi kutatuliwa. Vema. Basi kama lingetukia, ni wangapi wenu wangeamini ilikuwa ni Kristo, Roho Mtakatifu, sawasawa na nini basi? Vema, basi mpokeeni tu.

Lakini mimi na yeye, pamoja, hatujawahi kuonana maishani mwetu.

221 Sasa, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa iweni na kicho, iweni katika maombi. (Kwa utulivu, pamoja na kinanda.)

222 Sasa, mama, ninataka kuzungumza nawe kama tu Yesu alivyozungumza na yule mwanamke. Sasa, huenda uko hapa kwa ajili ya ugonjwa, huenda uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, huenda, sijui, mnaona, huenda ikawa ni mambo ya kifedha. Mi—mimi . . . Wewe ni mwanamke tu aliyesimama hapa. Hivyo ndivyo yule mwanamke alivyokutana na Bwana wetu.

223 Sasa, Naye akaongea naye kwa kitambo kidogo. Sasa, inakubidi kuchukua neno langu kwa ajili ya jambo hili, nisingeweza kuthibitisha hili kwa Maandiko. Lakini alikuwa na haja ya kupitia Samaria, Naye alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha, kwa hiyo hapana shaka ilikuwa hivi. Yeye, Baba alimtuma huko Samaria. Vema, jambo pekee alilojua, kufanya, lilikuwa ni kwenda Samaria. Alifikiri angekuwa peke yake, kwa hiyo akawatuma tu wanafunzi. Akangojea, mwanamke akaja, kwa hiyo huenda huyo alikuwa ndiye. Kwa hiyo akaketi pale, na kuanza kuzungumza naye. Alikuwa akifanya nini? Kuwasiliana na roho yake.

224 Sasa, kama Yeye angalienda huko chini, na kusema, “Mimi ndiye Masihi, mi—mimi ndiye Masihi,” ingekuwa afadhali mwanamke huyo aseme. Mnaona? Kumwacha ajitangaze Mwenyewe kwa mwanamke huyu. Mnaona? Mungu hufanya kazi kwa njia za ajabu. Mnaona? Naye akamwambia mwanamke huyo jambo fulani, lililokuwa maishani mwake.

Vema, akasema, “Huna budi kuwa ni nabii. Ninajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia jambo hili, Yeye alisema atafanya mambo haya.”

Yesu akasema, “Mimi Ndiye.” Sasa, Yeye aliahidi kazi zile zile, na hasa sana katika wakati huu.

²²⁵ Sasa, ka—kama ulikuwa mgonjwa, nami nikasema, “Nina karama ya uponyaji wa Kiungu,” karama ya uponyaji wa Kiungu si kitu ila imani katika uponyaji wa Kiungu, ni hivyo tu, iweni na imani. Kila mtu anayeamini katika uponyaji wa Kiungu ana karama ya uponyaji wa Kiungu, maana ni hivyo tu.

²²⁶ Sasa, hilo haliwafanyi kuwa mponyaji wa Kiungu, si zaidi ya vile inavyomfanya mtu anayeamini katika wokovu mwo—mwokozi wa Kiungu. Mnaona? Ni ninii tu, yeye anauamini. Ninauamini, pia, bali mimi si mtu mwenye kipaji kama baadhi ya hawa watu, kama Jack Coe, na wengi wa hao ndugu walivyokuwa, halisi tu...Nadhani wao, Mungu huwashughulikia katika njia zao, na Ndugu Roberts katika njia zake, nami kwa njia yangu; tuna huduma tu, hivyo tu.

²²⁷ Mungu aliweka kanisani mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, wachungaji. Hivyo tu. Halafu karama tisa za kiroho kanisani.

²²⁸ Sasa, unasema, “Ndugu Branham, unajaribu kufanya nini?” Ninajaribu kuwasiliana na roho yako. Yesu alinituma kwenye mji huu, niliongozwa hapa. Sasa, huyu hapa mwanamke, kwa kuwa na namba kwenye kadi yake ya maombi, huko juu kabisa kwenye. . .Ninasahau mahali nilipoita, hamsini ama sabini na tano ama mahali fulani hapa, nasahau sasa ilikuwa ni wapi, ilitokea tu kwamba ulikuwa ndiye mwanamke aliyesimama hapo. Vema. Sasa, bila kufahamiana, sasa, ninajaribu kufanya nini? Kuwasiliana na roho yako.

²²⁹ Na kama Bwana Mungu. . .Kama ningesema nilikuwa na karama ya uponyaji, nikaweka mikono yangu juu yako, niseme, “Bwana asifiwe. Haleluya! Utapona.” Hilo lingekuwa sawa. Nenda uamini, utapona, ninaamini, Mungu ataiheshimu imani yako.

²³⁰ Lakini vipi kama Yeye akija na kukwambia jambo fulani ambalo—ambalo umekuwa, kisha akwambie kile utakachokuwa. Unajua kama ni, kile kilichokuwa, kama ni kweli ama si kweli, jambo ambalo umefanya maishani mwako, huko nyuma kabisa, ama—ama chochote Yeye afanyacho, ama kitu kama hicho, basi kingemfanya Masihi yeye yule. Kusanyiko halingekosea, wangeamini, na kulikubali tu. Sasa, na alijalie.

²³¹ Sasa, kama kusanyiko lingali linaweza kuisikia sauti yangu ile Nguzo ya Moto mnayoiona kwenye picha imesimama moja kwa moja kati yangu na huyu mwanamke. Ninamwona, anaondoka, anaonekana mdogo kwa miaka mingi kuliko vile anavyoonekana mwenyewe, akisimama karibu nami. Amerudi

kwenye... Amefanyiwa upasuaji wa namna fulani, na huo ulikuwa kwenye koo lake, ulikuwa ni tezi. Hiyo ni kweli. Kama hiyo—kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

²³² Vema, sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, hebu na tuzungumze tu na mwanamke huyu kwa muda mrefu zaidi kidogo, mnaona, muda mrefu zaidi kidogo, mnaona. Ili kwamba ninyi... Watu wanafikiri ulibahatisha hilo. Angalia kile kingine Yeye angesema.

²³³ Naam, ninamwona sasa, tena, ni upasuaji kwenye koo. Huo umekuwa muda mrefu uliopita, na kitu hicho kimerudi tena, unacho tena. Hiyo ni kweli. Lakini angalia amejificha kutoka kwa daktari, bali hawezi kujificha kutoka kwa Mungu, Mungu anajua pale pale alipo. Ni uhai, kuongezeka kwa seli zikikua, kukaba roho, kama tu vile ulivyokuwa mtoto mchanga katika tumbo la uzazi la mama yako ukikua, lakini hii haina umbo, inaenea tu, ni pepo, roho inayokaba. Hiyo ni kweli.

²³⁴ Ili upate kujua: Huyu hapo mwanamke aliyeketi papo hapo, ugonjwa wa koo, pia. Hiyo ni kweli. Uligusa nini? Sikujui, sivyo? Sijawahi kukuona maishani mwangu, lakini huo ndio unaougua. Mnaona, ninaweza kuhisi huyo ni roho mmoja akimwita huyo mwingine, namna hiyo, apate msaada, mnaona, namna hiyo, amehama, mnaona. Kama Roho Mtakatifu angeniambia wewe ni nani, ingekusaidia? Ingelisaidia hili kusanyiko? Bibi Harrison, unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Imani yako inakuokoa.

²³⁵ Je, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Sasa, hapa alisimama mwanamke akiwa na kadi ya maombi, huyo aliyeketi hapo kwenye kusanyiko, mnaona. Sasa, haiwezekani kabisa kwangu kufanya hivyo.

²³⁶ Unasema, “Ndugu Branham, niambie.” Siwezi kufanya hivyo, sijui. Wewe mguse tu upate kujua.

²³⁷ Mwanamke yule aliyeketi pale alikuwa akiomba, ndipo roho huyo... Hebu anza kuomba uone kitakachotukia. Liamini tu, usilitilie shaka, liamini tu kwa moyo wako wote uone tu litakalotukia, amini tu.

²³⁸ Hatufahamiani, tulizaliwa, labda, tumeachana kwa miaka mingi, lakini kama Bwana Mungu atanifunulia jambo fulani moyoni mwako, upate kujua ya kwamba Hilo ni—Hilo ni Neno Lake, kwamba Ujumbe huu ambao nimehubiri usiku wa leo, huo ni Neno Lake... Na kama Hilo linakaa moyoni mwangu, basi Neno la Mungu ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Hiyo ni kweli? Kama tu ilivyokuwa wakati alipofanyika mwili katika Mwana wa Mungu, Ni Kitu kile kile miilini mwetu, leo, Kanisa.

²³⁹ Kwa hiyo nisingeweza kufanya hivyo mwenyewe, inahitaji wewe kufanya hivyo, pia, kuwapeleka huko nje. Inahitaji mtu mwingine huko nje kuwa na upako uu huu. Mnaona? Huenda isininii... Itafanya kazi, lakini labda wao hawata—hawataweza

kuitangaza, kwa sababu hii ni karama. Mnaona? Nilipozaliwa, karama na miito, bila majuto, nilikuwa mtoto mdogo tu wa kiume, jambo lile lile lililotukia, moja kwa moja, kote maishani, bila majuto.

²⁴⁰ Wewe ni mgonjwa kwa sababu umekuwa ukishauriana na daktari kuhusu jambo fulani. Sawa. Na huo—huo ni ugonjwa wa koo, pia. Hiyo ni kweli. Na sasa, huu hapa uchanganuzi wake, wewe kuwa mwamuzi: Uko kwenye kijisanduku cha sauti, na ni kidonda ndani ya kijisanduku cha sauti. *Ulikuwa*, hauko sasa, imani yako imekuokoa...?...

Kuwa tu na imani.

²⁴¹ Hatufahamiani, mama, sikujui. Kama Mungu atanifunulia kile kilichokuleta hapa, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Utaamini? Ni ngiri. Ulikuwa na matatizo fulani, sivyo, lakini upasuaji wa daktari mpasuaji unaathiri uhai, kansa. Sasa umekuwa ni ngiri. Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Yeye alikuponya? Basi nenda, Mungu atakupua afya. Mungu akubariki.

²⁴² Kuwa na imani. Mnaamini? Huko nje kwenye kusanyiko, iweni tu na kicho kabisa. Sijali mko wapi. Na—nawaomba, kama ndugu yenu, katika Jina la Yesu Kristo kuamini hili kuwa ni kweli. Angalia kinachotukia. Omba tu, useme, “Bwana, jalia nikuguse Wewe,” uone kitakachotukia. Na—naamini... .

²⁴³ Sasa, hayo yananiacha dhaifu sana, dhaifu sana. Ni wangapi wangeweza kuelewa hilo? Hakika. Kama Mwana wa Mungu, mtu mmoja tu alimghusa, Naye akasema nguvu zilimtoka, vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Lakini inatangaza Yeye yupo hapa, inatangaza Uwepo Wake, Yeye yupo hapa. Mnaamini hilo, pia, mkisimama, pande zote hapa? Mnaamini? I—iweni tu na imani na mwamini.

²⁴⁴ Hebu kidogo. (Sasa, nitakapofikia kama tatu kati ya hizi, hebu nijulisheni, basi, nina mikutano mingine inayokuja.) Ha—hatufahamiani, sikujui, lakini unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kama ulikuwa umesimama hapa, na Bwana wetu alikuwa hapa katika umbo la kimwili... Yeye yupo hapa kiroho, kwa sababu ni Roho Mtakatifu aliyeshuka juu Yake kama Hua, na sasa anashuka juu yetu kama Moto.

²⁴⁵ Wewe ni mwaminio, simaanishi mwomba lifti, ninamaanisha mwa—mwaminio. Hiyo ni kweli. Basi unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kama ningeweza kukwambia kwa Roho wa Mungu kilichokuleta hapa, utaniamini? Uvimbe puani. Loo, hicho ni kitu kibaya sana! Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Lakini hayo si yote yaliyo moyoni mwako. Una kitu kingine moyoni mwako unachotaka nikuambie habari zake. Ana kidonda mguuni. Chukua lesa hiyo ambayo unapangusa machozi yako nayo ukaiweke juu ya hicho kidonda. Kitamwacha. Nenda ukaamini sasa.

²⁴⁶ U hali gani, bwana? Hatufahamiani. Sijawahi kukuona hapo kabla, nasi hatufahamiani. Lakini Mungu wa Mbinguni, Ambae alimfufua Mwanawe, Yesu Kristo, Ambaye alipaa Juu na kuwarudishia wanadamu vipawa, Naye akaweka ndani ya kanisa mitume, ambalo linamaanisha “mmishenari,” manabii, hilo linamaanisha “mwonaji,” wachungaji, wainjilisti, na kadhalika, Yeye angali anabaki Mungu. Kama Mungu atanifunulia kilicho shida yako, utanipokea kama nabii Wake, ama, kama mtumishi Wake? Utafanya hivyo? Vema, bwana.

²⁴⁷ Je, kusanyiko litafanya jambo lile lile? (Je, hawa ni watatu, bado, ama...? Hiyo ni ninii tu, vema, ninii tu, tunaye huyu hapa.) Kuna jambo la kigeni kumhusu huyu mtu, siwezi kulielezea bado, hebu Roho Mtakatifu alifunue ninapozungumza naye. Natumaini sauti yangu ni kubwa vya kutosha mnaweza kusikia.

²⁴⁸ Inapita... Sasa, sasa hii hapa inamjia huyu mtu. Huyu mtu yuko katika hali mbaya sana, yuko karibu na kufa. Ametiwa uvuli wa mauti kwa kansa, nayo hiyo kansa iko kwenye koo lake. Hiyo ni kweli. Mwajua, kuvuta sigara kunaathiri koo. Utaziacha? Uzirarue?

²⁴⁹ Jambo lingine, wewe si Mkristo, wewe ni mwenye dhambi. Je, utamkubali kama Mwokozi wako, kwa ajili ya nafsi yako? Ikiwa Mungu kwa...? Mtume Petro alikuja, alikuwa mwenye dhambi, pia. Kama Mungu atanifunulia jina lako, na kuniambia jina lako, kama alivyomwambia mtume Petro, utaamini ya kwamba ni Kristo, Mungu Yule anayekupenda, na anakuokoa sasa, kutoka...? Utaliamini neno langu kwamba dhambi zako zimesamehewa? Utaamini? Bw. Davidson, basi nenda nyumbani, ukapate afya.

Mwaminini Mungu. Ninaendelea kuhisi kitu fulani kikiingia huko kutoka mahali fulani, mnafikiri ninasoma mawazo yao, sisomi.

²⁵⁰ Hapa, gusa tu mkono wangu, mama. Kama nitaangalia *huku* na kukwambia shida yako, utajua kama ni kweli ama si kweli. Hiyo ni kweli? Basi kansa yako itaondoka kama utaamini. Utaamini? Inua mkono wako kama ndivyo ilivyo. Vema, basi nenda, uwe na imani.

²⁵¹ Njoo, mama. Utaamini, mama? Kwamba Mungu atanifunulia, ukiangalia huku, kilicho shida yako, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? [Dada huyo anasema, “Ninaamini wewe ni nabii.”—Mh.] Unaamini, kuwa nanii Wake... Asante, Dada. Basi nenda ukale chakula chako cha jioni, ugonjwa huo wa tumbo umekuacha.

Kama nikiwaambia kabla mama huyu hajaja? Alikuwa na jambo lile lile, ana tumbo lenye wasiwasi, umekuwa nalo kwa muda mrefu, nenda ukale. Kuwa na imani.

Unaamini ugonjwa wako wa mgongo umekuacha, uliyeketi hapo? Vema, basi nenda. Bwana asifiwe.

Wasikilizaji, msiwe na shaka, ninii tu. . .

Njoo, mama. Ugonjwa wa moyo, Mungu angeweza kuponya ugonjwa wake wa moyo. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

Mungu huponya yabisi kavu, pia. Ulijua hilo? Basi nenda ukaamini.

Njoo. Unaamini Mungu anaweza kuponya pumu yako na kukupa afya? Nenda ukishangilia, ukimshukuru Mungu.

Unaamini Mungu anaweza kuponya kisukari chako, na kukupa afya? Endelea, nenda.

Kama huyo mama mwingine aliponywa pumu, msichana mdogo kama wewe angeweza kuponywa hiyo, sivyo? Uh-huh. Usiwe na shaka, kuwa na imani.

Unaamini? Kusanyiko lote linakuwa kama maziwa kwangu.

²⁵² Mtu huyo aliyeketi hapo mwenye yabisi kavu, aliyeketi hapo akiniangalia, nililipata dakika chache zilizopita wakati mama huyo alipokuwa ameamini, imani yako inakuokoa, endelea.

Unaamini kwa moyo wako wote?

Unaamini Mungu anaweza kuponya hicho kisukari? Ulianza kuamka muda mfupi uliopita, ningeweza kukwambia wakati huo. Usijali, imekwisha.

²⁵³ Vipi kuhusu wewe uliyeketi karibu naye hapo, hiyo ilikubariki, pia? Mtu huyo aliyeketi karibu naye, unaamini Mungu ataponya hilo shinikizo kuu la damu, akupe afya? Vema.

Huyo mama aliyeketi karibu naye alikuwa na kisukari, pia. Unaamini Yeye atakuponya?

Vipi kuhusu wewe uliyeketi hapo mwishoni, uwekelewe mikono, unaamini utapona? Njoo hapa. Katika Jina la Bwana Yesu, nenda ukaponywe.

²⁵⁴ Unajaribu kujishikilia, kila mtu anakwambia hivyo, hata hivyo, lakini wasiwasi ni kitu kibaya sana. Umetaka mahali pa kuweka mguu wako, ili uweze kuanzia papo hapo. Hiyo ni kweli? Unamulikwa sasa, wasiwasi wako umekwisha. Nenda, amini.

Unaamini kwa moyo wako wote? Baadhi yenu huko nje ombeni, aminini.

²⁵⁵ Hapa, huyu hapa mwanamke ameketi mbele yangu, yeye anaomba, bali hajiombe mwenyewe, anamwomba mama yake, mama katika hospitali ya wendawazimu. Ulishangaa kama nilikuwa nikikuzungumzia, sivyo? Ulikuwa ukitaka niwasiliane. Sasa, kama ulikuwa ukimwomba mama yako, inua mkono wako. Huyu mama aliyeketi hapa. Hakika.

²⁵⁶ Ninakupa changamoto kuamini, ninakupa changamoto kuamini vyovyote utakavyo. Unaamini?

257 Ni wangapi wa, humu ndani...? Ni wangapi humu ndani wasiomjua Yesu kama Mwokozi wako, nawe ungetaka kumjua Yeye, sasa hivi, kama Mwokozi wako? Inua mkono wako. Unataka kumjua Yeye kama Mwokozi wako, simama kwa miguu yako. Ninyi mnaotaka kumjua Yeye kama Mwokozi, sasa hivi, kumkubali papa hapa wakati akiwepo, simameni kwa miguu yenu, kila mahali jengoni, simameni kwa miguu yenu.

258 Mnajua Yeye yupo, sivyo? Ninajaribu kuondoka kwenye madhabahu hii. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa kukusamehe kila dhambi, je, utamkubali Yeye, sio vile unavyojisikia, bali juu ya msingi kwamba alikufa kwa ajili yako, nawe unajua uko Mbele Zake sasa, nawe unaamini ya kwamba alikufa kwa ajili yako, nawe unamtaka awe Mwokozi wako, utamkubali Yeye juu ya misingi hiyo? Mwinulieni mikono yenu.

259 Baba wa Mbinguni, Wewe ulisema katika Neno ya kwamba “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Na watu hawa katika roho zao wanajua ya kwamba wamekosea, na kwa hiyo wamekukubali Wewe kama Mwokozi wao, ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawajalia hilo, sasa hivi, wamekukubali Wewe.

260 Wewe ulisema, “Yeye anijiaye Mimi sitamtupa nje kamwe. Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.” Ulisema katika Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Wao ni Wako, Baba, wao ndio ishara za mkutano huu.

261 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kama unaamini ya kwamba Mungu huyasikia maombi yangu, ninakutaka uje hapa, ondokeni moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa hapo ninyi mlioinua mikono yenu. Njoni papa hapa na msimame hapa kwa dakika moja, moja kwa moja madhabahuni, sogeeni moja kwa moja huku kwa dakika moja. Kila mtu anayemtaka Kristo sasa hivi, shuka moja kwa moja hapa njoo tu hapa.

Hapo, kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa
ajili ya...

Na kwamba Wewe umeniamuru nje Kwako,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!

262 Kila mshiriki wa kanisa usiyemjua Kristo kama Mwokozi wako, nawe unataka kumjua Yeye, kwa nini umkatae sasa hivi, unapoiona Hiyo, upo papa hapa, upo? Kama Mungu akiyasikia maombi yangu, na kuyafungua macho ya vipofu, na kuwafanya viwete kutembea, Yeye—Yeye atasamehe dhambi yako, pia.

263 Kama Yeye anaujua moyo wako, na kukwambia jukwaani kilichoko, Yeye ananiambia, huko nje, kungali kuna wengine wanaopaswa kuja. Yeye anazungumza nanyi, si lazima niwaite,

maana ninadhoofika sana hata siwezi kusimama hapa. Njoni upesi sana, sivyoy? kusudi isinibidi kungojea zaidi. Njoni, sasa hivi.

Jinsi tu nilivyo, wala singojei
 Kuiondolea nafsi yangu doa moja jeusi,
 Kwako Wewe, ambaye Damu Yako inaweza
 kusafisha kila doa,
 Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, (Vema,
 sasa)...naja! Naja!

Jinsi tu nilivyo, Wewe utanipokea,
 Utanikaribisha, unisamehe, unitakase,
 unipokee;
 Kwa sababu ninaahidi ninaamini,
 Ee Mwana-kondoo...

Njoo, ndugu yangu. Njoo, dada yangu.

...naja! Naja!

Jinsi tu nilivyo, Wewe utanipokea,
 Utanikaribisha...

²⁶⁴ Njoni, kila mtu, njoni sasa. Usingoje, kama huna hakika sana, njoo sasa. Yuko papa hapa jukwaani. Mbele za Mungu, ninasema kweli, ile Nguzo ya Moto, yule Malaika wa Mungu, Yeye anayejua moyo wa kila mtu, yupo papa hapa sasa.

...Mwana-kondoo wa Mungu...

²⁶⁵ Kamwe hutakuwa karibu zaidi mpaka utakapomwona Yeye akija.

...mimi...

²⁶⁶ Kama kuna swali lolote moyoni mwako, njoo sasa.

...nilivyo, singojei
 Kuiondolea nafsi yangu doa moja jeusi,
 Kwako Wewe, ambaye Damu Yako inaweza
 kusafisha...(Waweza—waweza kuja
 kutuombea?)
 Ee Mwana-kondoo...

...pokea,
 Utakaribisha...

Njoo, maskini mama...?... 

61-0224 Msiogope
Fairgrounds Auditorium
Tulare, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org